Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo



**Ni mchuano mkali matokeo darasa la saba**

Uk. 2

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00087 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Oktoba 30 - Novemba 5, 2024 |

**Wakulima vijana wa vitunguu wasaidiwa** Uk. 5



**Utafiti mpya wa ngozi kupunguza kuzeeka** Uk. 7



**Mvutano ni mkali baina ya Trump na Kamala**



Uk. 15

### MKUTANO WA WENZA WA MARAIS AFRIKA:

# Dk. Samia awapa neno nishati safi ya kupikia

- **Ataka ushawishi wa joto kwa wenza wao**

Uk.4



Rais Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na Mama Fatma Karume pamoja na Mama Siti Mwinyi, waliposhiriki katika Mkutano wa 11 wa Merck Foundation Africa Asia Luminary uliofanyika jijini Dar es Salaam, jana.
Picha ya chini: Akiwa na wenza wa wakuu wa nchi mbalimbali barani Afrika, mara baada ya ufunguzi wa Mkutano huo.



## ... Amlilia Jenerali Musuguri

Uk.4



Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya maisha yake ya miaka 104, ambapo miaka 46 kati ya hiyo ameitumikia nchi yetu kwa weledi, umahiri, kujituma, ushujaa, nidhamu na kwa mafanikio ya hali ya juu...

## ... Atua nchini Marekani kushiriki mjadala wa Kimataifa

Uk.2

rifaly

Habarika kidijitali! Soma gazeti la Uelekeo ndani ya Rifaly!

Scan to download Rifaly

www.rifaly.com

# Rais Dk. Samia atua Marekani kushiriki mjadala wa Kimataifa



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, jana aliatarajia kuondoka nchini kuelekea Des Moines, Iowa, nchini Marekani kuhudhuria Mjadala wa Kimataifa wa Norman E. Borlaug ulioandaliwa na Taasisi ya World Food Prize Foundation ya nchini humo.

Mjadala wa Kimataifa wa Norman E. Borlaug hufanyika kila mwaka na kuhudhuriwa na viongozi, wataalamu, watu mashuhuri, watunga sera, hususan za kilimo, lishe na usimamizi wa rasilimali. Shabaha ya majadiliano hayo ni kutafuta suluhu ya changamoto ya upatikanaji wa chakula duniani, ambayo inachochewa na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, Rais Dk. Samia ni miongoni mwa Marais wanne kutoka Afrika, waliopewa heshima ya kushiriki na kuchangia kwenye mjadala huo wenye kaulimbiu isemayo: Mbegu za Fursa: Kuunganisha Vizazi na Kustawisha Diplomasia (Seeds of Opportunity: Bridging Generations and Cultivating Diplomacy). Viongozi wengine watakaoshiriki ni kutoka nchi za Sierra Leone, Madagascar na Nigeria.

Mbali na Mjadala huo, taarifa ilisema Rais Dk. Samia pia atashiriki hafla ya utoaji tuzo ya World Food Prize kwa mwaka 2024 kwa watu wenye mchango mkubwa katika sekta ya kilimo, ikiwa ni mwendelezo wa kumuenzi Hayati Dkt. Norman E. Borlaug aliyehamasisha usalama wa chakula duniani kwa watu wote.

Sambamba na kushiriki kwenye majadiliano hayo, Rais Dk. Samia atakutana na kufanya mazungumzo (round tables discussion) na viongozi kutoka Serikali na sekta binafsi ya Marekani, hususan waliopo kwenye sekta ya kilimo kwa lengo la kujadili uwekezaji katika sekta hiyo na kuongeza mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo ambayo ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini nchini.

---

# Jenerali Mstaafu Musuguri afariki dunia





**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Majeshi Mstaafu, Jenerali David Musuguri, amefariki dunia jijini Mwanza alipokuwa akipatiwa matibabu.

Mwili wa Jenerali Musuguri aliyefariki dunia jana, unatarajiwa kuzikwa nyumbani kwake, Butiama mkoani Mara baada ya taratibu kukamilika.

Jenerali Musuguri aliyezaliwa Januari 4, 1920 Butiama mkoani Mara, aliitumikia nchi katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kuanzia mwaka 1942 hadi 1988, akihitimisha uongozi wake kama Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi kati ya mwaka 1980 na 1988.

Alianza kazi yake kijeshi katika King's African Rifles (KAR) na Tanganyika Rifles na baadaye Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Jenerali Musuguri aliongoza majeshi ya Tanzania katika vita dhidi ya Idi Amin Dada wa Uganda mwaka 1978, baada ya uvamizi wa eneo la Kyaka, mkoani Kagera.

Mapambano na vita alivyoshiriki ni pamoja na Vita Kuu ya Pili ya Dunia, Battle of Madagascar (1942), Vita vya Kagera au Battle of Simba Hills.

---

**MATOKEO DARASA LA SABA:**

# Ni mchuano mkali

- **Wavulana ufaulu 81.85%, wasichana asilimia 80.05**

**Na Mwandishi Wetu**

MATOKEO ya ufaulu kwa wanafunzi wa darasa la saba, yanaonesha kuwepo kwa mchuano makali kati ya wavulana na wasichana.

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), Dk. Said Mohamed jana imeonesha kuwa wavulana waliofaulu ni 449,057 sawa na asilimia 81.85 na wasichana ni 525,172 sawa na asilimia 80.05.

Taarifa hiyo ilisema mwaka jana, wavulana waliofaulu walikuwa asilimia 80.59 na wasichana walikuwa asilimia 80.58.

Alisema ufaulu wa jumla kwa mwaka huu umeonesha kuongezeka kwa asilimia 0.29.

Kuhusu ufaulu wa somo la Kiswahili, alisema ni mzuri ambapo asilimia 86.58 ya watahiniwa wamefaulu huku somo la Kiingereza ukiwa ni asilimia 43.48.

Sambamba na hayo, alisema NECTA imezuia kutoa matokeo ya wanafunzi 418 ambao waliugua au kupata matatizo mbalimbali na kushindwa kufanya kwa idadi kubwa ya masomo yote.

"Watahiniwa hao ambao matokeo yao yamezuiwa tumewapa fursa ya kurudia na kufanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (PSLE) mwaka mwakani kwa mujibu wa kifungu cha 32 (1) cha Kanuni za Mitihani," alisema.

Alisema watahiniwa 45 waliofanya udanganyifu wamefutiwa matokeo yao na 16 walioandika lugha za matusi kwenye karatasi zao za majibu nao wamefutiwa matokeo kwa mujibu wa sheria.

Aidha, NECTA inazipongeza kamati zote za uendeshaji Mitihani za Mikoa na Halmashauri/ Manispaa,wakuu shule, wasimamizi na wasahihishaji wa mtihani huo kwa kazi kubwa na nzuri waliyojfanya katika kutekeleza jukumu la uendeshaji wa mtihani huo.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), Dk. Said Mohamed.

# Rais Dk. Samia akifungua mkutano wa 11 wa Merck Foundation Africa Asia Luminary jijini Dar es Salaam jana















# Dk. Samia awapa neno nishati safi ya kupikia

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amewahamasisha wenza wa Marais Afrika, kuwashawishi waume zao (Marais) waichukue ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia kama kipaumbele katika utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema hayo katika hotuba yake ya kufungua mkutano wa 11 wa Taasisi ya Hisani ya Merck Foundation Afrika-Asia uliofanyika jijini Dar es Salaam jana.

Kuhusu ushawishi, Rais Dk. Samia alielezea mfano wa makubaliano kati ya Jua na upepo kuhusu nani anaweza kumshawishi msafiri avue koti alilovaa.

Alisema upepo alianza, lakini kila ulipoongeza kasi, ulimsababisha msafiri kufunga vizuri koti lake hali ambayo ilikuwa tofauti kwa jua ambaye kila alipoangaza na kuongeza joto zaidi, msafiri alilazimika kwa hiari kuchojoa koti lake.

Kwa hiyo, Rais Dk. Samia aliwasihi wake wa Marais kuchukua hoja ya nishati safi ya kupikia kwa ushawishi mkubwa, uzuri na yenye joto kwa waume zao.

Alisema wakifanikiwa kufanya hivyo, Marais wenzake wataipa kipaumbele hoja hiyo na kuwa ajenda muhimu ya kuwasaidia wanawake wenzao katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Kwa mujibu wa tovuti ya Wizara ya Nishati, ifikapo mwaka 2030, watu milioni 300 Barani Afrika, watakuwa wanatumia nishati safi ya kupikia huku Rais Dk. Samia akiwa kinara katika kuhamasisha ajenda ya nishati safi ya kupikia.

Mapema katika ufunguzi wa mkutano huo, Rais Dk. Samia alisema serikali anayoiongoza, imetekeleza miradi mingi ya maendeleo kama afya, maji na elimu kwa kujenga majengo mapya na ya kisasa na kubadilisha mitaala ambayo sasa inazingatia ujuzi.

Aliishukuru Merck Foundation kwa mchango wa kusomesha wataalamu katika sekta ya afya na pia kwa kupitia programu ya Linda ambayo inatoa mchango mkubwa kuelimisha mtoto wa kike.

Aliihakikishia taasisi hiyo kuwa Tanzania itaendelea kushirikiana nayo katika kufanikisha majukumu yake.

Merck Foundation pamoja na mambo mengine, inajikita zaidi katika kugharimia mafunzo kwa wataalamu wa afya kwenye maeneo ya saratani kwa watoto (paediatric oncology) matibabu ya saratani kwa upasuaji (surgical oncology) matibabu ya saratani kwa utabibu (medical oncology).

Mafunzo kwa wataalamu hawa yanatolewa kwa muda wa mwaka mmoja hadi mitatu, lengo kuu likiwa ni kuboresha upatikanaji wa huduma zote zinazohusu saratani.

Pia wanajikita katika kuwajengea uwezo kinamama wenye matatizo ya ugumba kwa kuhakikisha wanapata taarifa sahihi zinazohusiana na matatizo ya ugumba.

Mkutano huo unahudhuriwa na watu kutoka nchi mbalimbali, ambapo miongoni mwao ni wenza wa wakuu wa nchi 15 za Afrika na Asia, watunga sera, wanataaluma, watafiti na wanahabari wa masuala ya afya kutoka nchi mbalimbali duniani.

# ...amlilia Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Musuguri

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan ametoa pole kwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob John Mkunda, makamanda, wapiganaji wastaafu, wapiganaji walio katika utumishi, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania kwa kuondokewa na shujaa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Mstaafu Jenerali David Bugozi Musuguri.

Katika taarifa yake kupitia akaunti yake rasmi ya Instagram jana, Rais Dk. Samia alisema anamwombea kwa Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

"Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya maisha yake ya miaka 104, ambapo miaka 46 kati ya hiyo ameitumikia nchi yetu kwa weledi, umahiri, kujituma, ushujaa, nidhamu na kwa mafanikio ya hali ya juu, akiishi kiapo chake cha kuwa tayari kuutoa uhai wake kwa ajili ya ulinzi wa Taifa letu," alisema.

Alisema marehemu Jenerali Musuguri amewaachia Watanzania mfano bora wa utumishi wa umma utakaoendelea kuwa mwanga ndani na nje ya majeshi ya Tanzania.



# Wakulima vijana wa vitunguu `wapigwa jeki'

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC), imekabidhi mtambo wa umwagiliaji wenye thamani ya Sh. 4,236,000 kwa Jacob Davis na wenzake wawili wanaojishughulisha na kilimo cha umwagiliaji ambapo kwa sasa wamejikita kuzalisha vitunguu katika Kijiji cha Nakahengwa katika Halmashauri ya Songea Vijijini.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, Mkuu wa Wilaya ya Songea, Kapenjama Ndile, alisema Septemba 17, mwaka huu, Waziri wa Kilimo aliahidi kuwasaidia vijana hao alipotembelea shamba lao akiwa ameongozana na Mkurugenzi Mkuu wa NIRC, Raymond Mndolwa pamoja viongozi wengine.

Waziri Bashe alivutiwa na kilimo hicho ambapo vijana hao walieleza changamoto zinazowakabili katika kilimo hicho ikiwa ni pamoja na kukosa miundombinu ya uhakika ya umwagiliaji, hali inayowafanya washindwe kupanua wigo wa kulima mashamba makubwa kutokana na hali duni ya kiuchumi.

Awali, wakulima hao vijana walikuwa wakilazimika kutumia jenereta bovu kuvuta maji ya kumwagilia shamba hilo.



Baada ya Waziri Bashe kupitia katika kijiji hicho na kujionea shamba hilo, alimwagiza Mkurugenzi NIRC kuwanunulia vijana hao mtambo ambao umekamilika kila kitu, ahadi ambayo imetekelezwa.


Kwa sasa vijana hao wanalima ekari tatu za vitunguu na soko lao kubwa ni miji ya Songea na Mbinga ambapo mji wa Songea pekee unahitaji tani 50 za mboga mboga kwa siku.

Vijana hao wameahidi kupanua zaidi shamba lao, lengo ikiwa ni kuvuna zaidi ili walishe nchi nzima.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO



## Ubora bidhaa sokoni udhibitiwe

Kuna tatizo la ubora wa mazao katika masoko yetu, likiwemo soko la Stereo Temeke. Wachuuzi wanaleta sokoni bidhaa ambazo zimelazimishwa kuiva, wenyewe wanaita kupepea. Kinachofanyika inaelezwa mara nyingi wanatumia moto kufanya mazao, hususani matunda ambayo hayajaiva au kukomaa kuonekana kama yamekomaa na kuiva!

Kwa hiyo kuna maembe, ndizi, mapapai na matunda mengine kadhaa ambayo unaweza kuona yakimeremeta kama yameiva lakini ukila unashangaa kuona jinsi lisivyo na ladha yoyote.

Ni vyema, kama ambavyo machinjioni kuna maofisa wa afya wanaochunguza nyama ili itemize vigezo, ni wakati mwafaka kwenye masoko kuwe pia na maofisa wanaopima ubora wa bidhaa.




MAONI YA MHARIRI

# Tuwe na mkakati kila kijiji kuwe na matumizi bora ya ardhi

Shabani Mruma, Ofisa wa Upimaji Ardhi, Jumatatu hii akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Kaimu Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Tanga, alisema anatamani kuona vijiji vyote nchini vikiwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi, hatua itakayofanya kila kipande cha ardhi kujulikana matumizi yake.

Alieleza kuwa ili kijiji kiwe na mpango wa matumizi bora ya ardhi, ni lazima kipimwe, mipaka yake ijulikane, na maeneo mbalimbali ya kijiji yapangwe kulingana na mahitaji; kama vile eneo la msitu wa kijiji, mashamba, makazi, huduma za kijamii, na maeneo ya uwekezaji.

Mruma alishauri halmashauri nchini zitenge fedha kila mwaka kwa ajili ya kupanga matumizi bora ya ardhi. Aliyasema haya huku akipongeza mradi wa IFBEST (Suluhisho la Ujumuishaji wa Misitu na Nishati Endelevu ya Tungamotaka Tanzania), ambao umeleta matumizi bora ya ardhi katika baadhi ya vijiji, hivyo kusaidia kumaliza migogoro mingi ya ardhi, ukiwemo mgogoro uliodumu kwa miaka 22 baina ya vijiji vya Lusane na Kitingi wilayani Kilindi.

Mradi wa IFBEST, unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) kupitia Wizara ya Fedha ya Tanzania, unalenga vijiji 13 kwenye wilaya nne za Mkoa wa Tanga; Kilindi, Pangani na Mkinga.

Parakole Leteto, Mwenyekiti wa Wafugaji wa Kata ya Tunguli na mkazi wa kijiji cha Lusane, anaeleza kuwa wakati wa mgogoro wao, mtu angeweza kuamka na kukuta njia ambayo mifugo inapitishwa kwenda malishonui au mnadani imegeuzwa kuwa shamba!

Natus Manumbu, Mkuu wa Maendeleo ya Ardhi wa Halmashauri ya Kilindi, anasema kwamba kijiji ambacho hakina mpango wa matumizi bora ya ardhi kinakabiliwa na migogoro baina ya kijiji na kijiji, au ndani ya kijiji, na pia kuna uwezekano mkubwa wa misitu kuvunwa kiholela.

Anasema wanegetamani kupima mipaka ya vijiji vyote 102 vya Wilaya ya Kilindi ili viwe na matumizi bora ya ardhi, lakini wanashindwa kufanikisha azma hiyo kutokana na ufinyu wa bajeti, na kwa sasa wamemudu kupima vijiji 15 pekee.

Napoleon Mlowe, Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Mazingira wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, anasema wameanza kutenga shilingi milioni 16 kwa ajili ya kuhamasisha vijiji vingine kufuata mfano wa mradi wa IFBEST katika kupanga matumizi bora ya ardhi na kulinda misitu.

Tunashauri halmashauri ziwe na mpango wa kuwezesha angalau kijiji kimoja kila mwaka kuwa na matumizi bora ya ardhi pamoja na kuimarisha ulinzi shirikishi wa misitu ya jamii (CBFM).

Kutokana na manufaa ya jambo hili, tunashauri pia serikali kuu kuliangalia kwa umakini zaidi. Yaani, kama ambavyo serikali imeweza kusambaza umeme katika vijiji vyote 785 mkoani Mtwara, tusikie siku moja vijiji vyote kila mkoa vikiwa na matumizi bora ya ardhi.

Hamid Yassin
JICHO LANGU
0768 888 787

# Hakuna ubishi, Dk. Samia ameimarisha demokrasia

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel John Nchimbi, ameithibitishia Jumuiya ya Kimataifa kuwa masuala ya demokrasia na haki za binadamu yataendelea kuimarika zaidi nchini Tanzania chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Balozi Nchimbi aliyasema hayo alipokutana na Balozi wa Uturuki nchini Tanzania, Dk. Mehmet Güllüoğlu, Balozi wa Morocco, Zacharia El Goumir, pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Sera na Tathmini wa Taasisi ya Misaada ya Marekani (MCC), kwa nyakati tofauti, Jumanne ya Oktoba 15, 2024.

Katika mazungumzo hayo yaliyofanyika Ofisi Ndogo ya Makao Makuu ya CCM, Lumumba, jijini Dar es Salaam, Balozi Nchimbi amesema katika kipindi cha uongozi wa serikali ya Awamu ya Sita, hatua kubwa imefikiwa katika kuimarisha demokrasia, utawala bora, uchumi na haki za kiraia.

Mazungumzo hayo ya Balozi Nchimbi na mabalozi wa nchi hizo, pamoja na taasisi ya MCC, yalilenga kuboresha uhusiano katika nyanja mbalimbali, zikiwemo siasa, kilimo, teknolojia, elimu, na michezo, kwa lengo la kuleta maendeleo ya pamoja kwa wananchi wa pande zote.

Naam; haya aliyozungumza Dk. Nchimbi hayahitaji kuvaa miwani ili kuyaona, kwani yako wazi kabisa kwamba demokrasia na haki za binadamu zimetamalaki hapa Tanzania.

Vyama vya siasa vimepewa uwanda mpana wa kufanya siasa katika kipindi hiki cha miaka mitatu na nusu ya uongozi wa Dk. Samia, madai mengine kinyume na ukweli huu ni zile siasa zetu za kupinga kila kitu!

> Si hivyo tu vyama vya siasa vya upinzani, bali hata hao mabalozi na taasisi hizo za kimataifa zinatambua kuwa, Tanzania hii ya Dk. Samia si ile ya Awamu ya Tano ambayo ilipiga marufuku kufanya siasa nyakati ambazo si za chaguzi.

Viongozi wa vyama hivyo vya siasa hata kama wanapinga hadharani, lakini kwenye mioyo yao na vikao vyao ndani naamini huwa wanakiri ukweli huu.

Si hivyo tu vyama vya siasa vya upinzani, bali hata hao mabalozi na taasisi hizo za kimataifa zinatambua kuwa, Tanzania hii ya Dk. Samia si ile ya Awamu ya Tano ambayo ilipiga marufuku kufanya siasa nyakati ambazo si za chaguzi.

Yapo matukio kadhaa ambayo viongozi wa vyama vya siasa vya upinzani wanayazungumzia kama ukosefu wa demokrasia na haki za binadamu, kama vile masuala ya upoteaji na madai ya kutekwa kwa wanachama wao.

Haya matukio ni magumu kuyathibitisha kwa maneno ya blaablaa bila vyombo vya dola na mahakama zetu kuyathibitisha kwamba yana uhusiano wa moja kwa moja na mkono wa Serikali. Hivyo hayawezi kumchafua Dk. Samia.

## Wasiliana nasi

| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255784122020 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |

# Utafiti mpya wa ngozi kusaidia kupunguza kuzeeka



UGUNDUZI wa kisayansi uliofanywa na timu ya kimataifa ya watafiti, hatimaye inaweza kuwa na matokeo muhimu kupunguza kasi ya dalili za kuzeeka.

Timu ya wanasayansi imegundua jinsi seli za ngozi zinavyotokana na seli zinazoweza kuzalisha seli zaidi zinazofanana nazo (au sterm cells) katika mwili wa binadamu, na timu hiyo hata imeweza kuzalisha sehemu ndogo za ngozi katika maabara.

Utafiti huo ulikuwa sehemu ya mpango mpana wa kujifunza jinsi vipengele vyote vya mwili wa binadamu vinajengwa katika kiwango cha seli.

Mbali na kupunguza kasi ya mchakato wa kuzeeka, matokeo ya utafiti yanaweza pia kutumika kuunda ngozi bandia kwa kupandikiza na hivyo kuzuia makovu.

Mradi unaojulikana kama The Human Cell Atlas ni mojawapo ya mipango ya kabambe zaidi katika biolojia.

Mradi huo ni wa kimataifa,

> **Kama tunaweza kuelewa jinsi seli zinavyobadilika kuanzia mapema hadi kuzeeka katika utu uzima, basi tunaweza kujiuliza: tunawezaje kufufua viungo, tunawezaje kufanya moyo kuwa wa umri mdogo, tunawezaje kuifanya ngozi kuwa changa?"**

lakini kituo chake kiko katika Taasisi ya Sanger huko Cambridgeshire, Uingereza.

Kwa mujibu wa mmoja wa viongozi wa mradi huo, Profesa Muzlifa Haniffa, utafiti unaofanywa ndani ya mfumo wake utawasaidia wanasayansi siyo tu kutibu magonjwa mbalimbali, lakini pia kutafuta njia mpya za kudumisha afya zetu kwa muda mrefu na labda, hata muonekano wa ujana zaidi.

"Ikiwa tunaweza kudhibiti ngozi yetu na kuzuia kuzeeka, tutakuwa na makunyanzi machache,"Profesa anasema. "Kama tunaweza kuelewa jinsi seli zinavyobadilika kuanzia mapema hadi kuzeeka katika utu uzima, basi tunaweza kujiuliza: tunawezaje kufufua viungo, tunawezaje kufanya moyo kuwa wa umri mdogo, tunawezaje kuifanya ngozi kuwa changa?"

Bila shaka, bado hii ni njia ndefu, lakini watafiti pia hawakomei hapo, kwani wanaendelea na utafiti wao, ikiwa ni pamoja na kuelewa ni

Inaendelea uk. 8



**Mguu wa binadamu unakua, na jeni zinazohusika na malezi ya mifupa, misuli na mifupa laini inayounganisha viungo vya mwili inayoonekana kama nukta za rangi.**

# Utafiti mpya wa ngozi kusaidia kupunguza kuzeeka

>>>Inatoka Uk. 7

jinsi gani seli za ngozi zinavyokua katika kiinitete katika hatua za mwanzo za maendeleo ya binadamu.

Wakati yai linaporutubishwa kwa mara ya kwanza, seli zote za binadamu ni sawa. Lakini ndani ya wiki tatu, jeni fulani ndani ya seli asilia zikisambaza maagizo ya utaalam na mkusanyiko ili kuunda sehemu mbalimbali za mwili wetu.

Watafiti wameweza kujua ni jeni gani, kwa wakati gani na katika maeneo gani yanaundwa ili kuunda kiungo kikubwa cha binadamu - ngozi.

Jeni zenye muundo wa machungwa huunda uso wa ngozi. Jeni za rangi ya manjano huamua rangi yake, lakini kuna nyingine nyingi ambazo huunda miundo inayotengeneza nywele, jasho, na kuzilinda dhidi ya ushawishi wa nje.

Kimsingi, wanasayansi wamepewa seti ya maagizo ya kuunda ngozi ya binadamu na wamechapisha maagizo haya katika jarida la Nature. Ikiwa unajifunza kusoma maagizo haya, uwezekano wa ajabu utafunguliwa mbele yako.

Kwa mfano, wanasayansi tayari wanajua kwamba tishu za kiinitete huponya bila kuacha makovu.

Seti mpya ya maelekezo ina habari juu ya jinsi hili linavyotokea, na maarifa haya yanaweza kusaidia kujaribu kubaini athari kwa ngozi ya watu wazima, kwa mfano wakati wa upasuaji.

Ugunduzi mwingine muhimu ni kwamba seli za kinga zina jukumu muhimu katika utunzaji wa mishipa ya damu katika ngozi, na wanasayansi waliweza kunakili maagizo ya jeni yanayofanana katika maabara.

Walitumia mchanganyiko maalumu kuchochea na kuzima jeni kwa wakati na mahali sahihi, na hivyo kukuza ngozi bandia kutoka kwa seli asilia katika maabara.

Hadi sasa, wamezalisha tu sehemu ndogo na nywele chache.

Profesa Haniffa anasema lengo la mwisho, ni ukamilifu wa teknolojia.

"Kujua jinsi ya kutengeneza ngozi ya binadamu, tunaweza kuitumia kutibu wagonjwa wenye majeraha ya kuungua na kufanya upandikizaji wa tishu," anasema.

"Mfano mwingine ni kama tunaweza kutengeneza nywele, tunaweza kukuza nywele katika watu wenye upara."

Ngozi iliyokuzwa na maabara, pia inaweza kutumika kujifunza magonjwa ya ngozi ya ya kuzaliwa na kupima matibabu mapya ya hali hizi.

Maelekezo ya kuchochea na kuzima utendaji wa jeni, hutumwa katika kiinitete na kuendelea kufanya kazi baada ya kuzaliwa na kuwa watu wazima, kuruhusu viungo na tishu zote kukua.

Mradi wa The Human Cell Atlas umechambua seli milioni 100 kutoka sehemu mbalimbali za mwili katika kipindi cha miaka minane tangu uanzishwe.

Matokeo yake, atlases mbaya za ubongo na mapafu ziliundwa na wanasayansi sasa wanaendelea kufanya kazi kwenye figo, ini, na moyo.

Hatua inayofuata, kwa mujibu wa profesa wa Chuo Kikuu cha Cambridge Sarah Teichman, ambaye ni mmoja wa waanzilishi na viongozi wa mradi huo, ni kuchanganya seli binafsi katika mfumo mzima wa mwili.

"Ni jambo la kufurahisha sana kwa sababu inatuwezesha kuangalia mfumo mzima wa muundo wa utendaji wa mwili wa binadamu, na kuelewa binadamu kwa njia mpya," aliiambia BBC.

"Itasababisha vitabu vya kiada kuandikwa upya juu yetu, tishu zetu na viungo na jinsi zinavyofanya kazi."BBC.





> Kujua jinsi ya kutengeneza ngozi ya binadamu, tunaweza kuitumia kutibu wagonjwa wenye majeraha ya kuungua na kufanya upandikizaji wa tishu.

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Oktoba 30 - Novemba 5, 2024 |

UTALII

AFYA

JAMII

Jarida hili haliuzwi



Lucia Zuberi: Mradi umetuletea elimu ya kuweka na kukopa pia umetuwezesha kugombea nafasi za uongozi.

# Tanga walivyoanza kunufaika na miradi ya utunzaji misitu

UK. 12 & 13

# Propaganda mfu zinavyowamaliza wapinzani




**Na Hamid Yassin**

KAULI wanazozitoa hivi sasa viongozi wa vyama vya upinzani hususani wale wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na kile cha ACT Wazalendo kwamba zoezi la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 'limenajisiwa', ni dhahiri shahiri kuwa, wameshakata tamaa ya kufanya vizuri kwenye uchaguzi huo sambamba na mipango ya kuing'oa CCM madarakani katika miaka ya hivi karibuni.

Kila kukicha kuelekea uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa vyama hivi viwili vikubwa vya upinzani vya Chadema na ACT Wazalendo vimekuwa vikiibuka na kauli hii ama ile, alimradi kuzua sitofahamu.

Katika mikutano na matamko yao ya sasa Chadema pia inazungumzia ushiriki wao kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa Novemba 27 mwaka huu huku wakitamba kufanya vizuri eti kama mizengwe haitakuwepo!

Chadema hawaeleweki na wepesi sana kusahau. Ni hivi karibuni tu hapa walidai hawatashiriki uchaguzi wowote bila kupatikana Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi?

Sasa zile kampeni zisizo rasmi walizofanya kwenye mikutano yao hapa Dar es Salaam, Kanda ya Ziwa na kule Kaskazini ya Tanzania kutaka kushinda uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na ule Uchaguzi Mkuu mwakani zinatoka wapi?

Ama tayari Katiba Mpya na Tume Huru wanazotaka wao zimeshapatikana?

Waache mazingaombwe ya kisiasa. Hivi sasa Watanzania wanaona kila kinachofanyika ndani ya taifa hili chini ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Dk. Samia.

Wanataka kushinda chaguzi mbele ya CCM, wamejipanga? Hebu wakumbuke kauli ya aliyekuwa mgombea wao wa urais mwaka 2015 hayati Edward Lowassa, halafu wakae chini wajitafakari!

Nakumbuka maneno ya aliyekuwa mgombea wa Chadema, marehemu Edward Ngoyayi Lowassa kwenye kampeni za Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 25 mwaka 2015 kuwa, wapinzani kama hawakushinda uchaguzi mkuu mwaka ule, basi wategemee kufanya hivyo baada ya miaka hamsini ijayo.

Hadi hivi karibuni, sikuwa naamini kwamba, marehemu Lowassa alimaanisha katika kauli yake ile zaidi ya kuwa lugha za kuwatahadharisha wapigakura wasifanye 'makosa' ya kumchagua aliyekuwa mgombea wa CCM wakati huo, hayati Dk. John Pombe Magufuli.

Kama kweli Lowassa alimaanisha katika kauli yake ile, basi hakuna haja ya kuwa na vyama vya upinzani kama Chadema katika medani ya siasa za hapa nchini, kwani miaka hamsini (nusu karne) kutoka wakati ule ni kipindi kirefu sana.

Sasa hivi Chadema inafanya kazi ipi iwapo wanaamini wangeshindwa kutumia fursa ya kuiondoa CCM mwaka ule madarakani basi hawataweza kuiondoa madarakani CCM kamwe katika kipindi hicho cha miaka 50.

*Inaendelea uk. 11*

# Propaganda mfu na wapinzani




*Inatoka uk. 10*

Na kwa kauli wanazozitoa hivi sasa viongozi wa Chadema, ni dhahiri shahiri kuwa, wameshakata tamaa ya kushinda huu uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuing'oa CCM madarakani katika miaka ya hivi karibuni.

Na walichofanya kwenye zile ziara zao za maandamano na haya matamko wanayotoa sasa ya juu ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, mimi naona ni kukipigia debe chama tawala kwa mlango wa uani!

Utatumia maneno yapi mapya ya kumpaka matope Dk. Samia mbele ya Watanzania hivi sasa? Kazi za Mama huyu wa Taifa zinaonekana na kila raia wa taifa hili wakiwemo wale wavaa miwani ya mbao kama baadhi ya viongozi wa Chadema.

Kila kukicha ni kuibuka na propaganda mpya, baada ya kujadili Uzanzibari wa Rais Dk. Samia, wakaja na habari za utekaji na upoteaji wa watu wakidai CCM, Serikali yake iliyo chini ya Dk. Samia na vyombo vya dola vina mkono katika matukio hayo.

Waziri Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry William Silaa akizungumza katika mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero za wananchi, uliofanyika hivi karibuni katika kijiji cha Makuro, Kata ya Makuro, Wilaya ya Singida, mkoani Singida, amesema Dk. Samia anawanyima usingizi wapinzani.

"Kazi aliyoifanya Rais Dk. Samia amewafanya hata wapinzani wakose cha kusema, hakuna cha kusema; kama kuna mtu hapa anafahamu sera yoyote imesemwa aniambie hapa." Aliongea Silaa.

Na kuongeza; "Ndiyo maana sasa hivi wamehamia watu wanatekwa, watu wanapotea, watu wanapotea, watu wanatekwa, na mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, bungeni alisimama mbunge mmoja wa upinzani akataka kwenye maswali ya Waziri Mkuu, aeleze serikali inachukua hatua gani kwenye suala la watu kupotea na kutekwa, Spika akasimama akasema tusizungumze bungeni kwa mihemko, kabla hujasema mtu anapotea au anatekwa lazima ujue nini kimetokea.

"Sisi wote hapa ni binadamu na hapa Makuro (Singida) nyinyi ni mashahidi, hapa aliwahi kuja mgeni mkampokea akaanza kujifanya yeye ni mtaalamu wa tiba (Mganga), watu wakaja hapa kutafuta tiba, wakaishia kuuawa, wakaishia kuzikwa, kule kwao kwenye familia zao wanasemaje?" Amehoji Silaa.

Aliwauliza wakazi hao wa Makuro kama wakienda kwa waganga huwa wanaaga ama wakishaona nyota imefifia, biashara haitoki, mama mapenzi nyumbani hayapo, wote hao wakienda kwa waganga wanaaga?

"Umekuja Makuro, umeenda kwa mganga matokeo yake amefanya alichokifanya, mauti yamekufika, amechimba shimo, amekufukia hivi kule kwenye familia za wale waliofukuliwa hapa Makuro wanasemaje? Wanasema ndugu zetu wamepotea, na wale wenye imani za upinzani wanasema ndugu zetu wametekwa, tumteke nani? Aliuliza Silaa.

Silaa alisema Tanzania ni moja ya nchi zenye amani na usalama kuliko nchi nyingine duniani. Jeshi la Polisi ni moja kati ya majeshi makini na yenye kufanya kazi nzuri ya weledi kabisa ndani ya taifa hili, akawataka wakazi hao wa Makuro kama wakiona ndugu yako haonekani, amepotea, waende katoa taarifa Kituo cha Polisi.

"Kwa hiyo lazima sisi kama Watanzania tunapoishi kwenye nchi ambayo tunajua tunaye Rais anayechapa kazi, aliyefanya mambo makubwa, lazima tujue kuna watu watakosa cha kusema, watatafuta ajenda za kudandia, nchi yetu ipo salama," alinena Silaa.

Walioeneza sumu ya ubaguzi, ya utekaji na mauaji si wengine bali ni wale wale viongozi wakuu wa Chadema, Mbowe, Makamu wake Lissu, Katibu wao Mkuu, John Mnyika na Godbless Lema ambao sasa wanakuja na madai ya 'kunajisiwa' kwa uchaguzi wa Serikali za Mitaa!

Nimewahi kuandika kwamba, Dk. Samia hachafuliki, narudia tena kamwe Chadema hawatafanikiwa kile wanachoita kukijenga na kuimarisha chama chao kwa ngonjera za kujaribu kumpaka matope rais wetu!

Changamoto kubwa inayoikumba Chadema na vyama vingine vya upinzani ni kukosa utambulisho kwenye makundi ya kijamii. Vile ambavyo vimeshindwa kusimamia itikadi zao zilizotumika kuvianzisha, vivyo hivyo havina shabaha kwa makundi mahsusi.

Hii ndiyo imekuwa sababu ya vyama hivi kuibuka na hoja za propaganda zisizoisha, mara mafisadi papa, mara huyu si Mtanganyika; propaganda muflisi zinazowafanya wagande sehemu moja bila kupiga hatua kwenye medani za siasa hapa nchini.

Bahati mbaya kwa vyama vya upinzani nchini ni kuwa vinachuana na chama kikongwe kinachoongoza dola kwa zaidi ya miaka 63 sasa.

Utaona kuwa CCM shabaha yake ilikuwa Watanzania wanyonge, yaani wakulima na wafanyakazi. Hata hivyo, baada ya kukaa madarakani muda mrefu, kilifaidika na kikawa chama cha watu wote, yaani hadi wafanyabiashara na vigogo wenye fedha.

Ni shida kubwa kwa chama cha siasa ambacho hakijawahi kushika dola, kikiwa hakijipambanui kimaudhui kuhusu wakulima, wafugaji, wavuvi na wote wenye kuendesha maisha kupitia fursa asilia. Chama kinakuwa hakina kundi linalokishika mkono.

Vyama vya upinzani vipo vingi, lakini wamachinga, mama lishe, waendesha bodaboda, bajaji na kadhalika hawaoni chenye kutafsiri vizuri changamoto zao ili wakione cha kwao. Uchaguzi unapofika wanaangalia mvuto wa mgombea na siyo chama.

Vita dhidi ya ufisadi ulikuwa utambulisho mkuu wa vyama vya upinzani kabla ya Uchaguzi Mkuu 2015. Utambulisho huo umeshapoteza mvuto na unaendelea kufutika kadiri Rais wa Awamu ya Sita, Dk. Samia Suluhu Hassani anavyopambana kurejesha nidhamu ya uwajibikaji na kupunguza kama si kuziba kabisa mianya ya rushwa.

Je, vyama kama Chadema havioni makundi mahsusi ya kutetea ili viungwe mkono na kupata utambulisho badala ya kuendeleza siasa za maji taka kila mwaka?

Ni hasara kubwa kwa chama cha upinzani kuifikiria dola wakati hakitafsiriki kwa unyoofu kwenye makundi ya kijamii. Matokeo yake watu wanaona vyama vipo sawa, isipokuwa vinatofautiana kuwa kingine kinatawala na vingine ni upinzani.

Chama cha upinzani kutegemea aina ya mgombea kwenye uchaguzi ili kukishinda chama tawala ni hasara kubwa. Chama kinatakiwa kiwe na mtaji mkubwa wa kuingia nao kwenye uchaguzi. Mtaji huo ni utambulisho wake kwenye jamii na namna kinavyopokelewa.

Chama hakipaswi kuingia kwenye uchaguzi na matarajio ya kamari. Kinapaswa kuwa na mtaji mzuri wa kisiasa. Na mtaji bora wenye nguvu ni utambulisho wake. Chama kikikumbatiwa na kundi kubwa au lenye mvuto na matokeo huvutia.

Kwa hiyo Chadema wajue yale wanayonena hivi sasa kwenye matamko yao ya propaganda, si ya kumbomoa Rais Dk. Samia bali ni kuzidi kumnadi yeye na chama chake CCM kuelekea uchaguzi wa mwaka huu Novemba 27 wa Serikali za Mitaa na hata ule Uchaguzi Mkuu wa mwakani!

*Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 au 0784 122 020.*

# Tanga walivyoanza kunufaika na miradi ya utunzaji misitu

"KULIKUWA na shida sana kuupokea huu mradi (wa kuleta Suluhisho la Ujumuishaji wa Misitu na Nishati Endelevu ya Tungamotaka Tanzania - IFBEST). Lakini sasa hawa wananchi huwaambii kitu kuhusu huu mradi," anasema Mtendaji wa Kijiji cha Lusane kilichoko katika Kata ya Tunguli, Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, Mbaraka Mazige.

Anasema kijiji hicho kilichoanza mwaka 1993, asilimia 95 ni wafugaji wa Kimasai ambao mwanzoni walipinga sana mradi huo lakini walipoolewa baada ya kupata elimu wakaukubali na sasa wameanza kunufaika nao.

Hii ni tofauti na wakazi wa Kijiji cha Mnkonde kilichoko katika Kata ya Msanja, wilayani Kilindi ambao huko nyuma walishakuwa na mradi kama huo na hivyo waliupokea bila kujiuliza mara mbilimbili na sasa wananufaika nao.

Kwa upande wa Kijiji cha Gendagenda kilichoko katika Kata ya Mgambo, katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, wao hawakuchelewa kuupokea mradi huo wakiamini utawasaidia kulinda msitu wa kijiji chao ambao hakukuwa rasmi lakini ulikuwa unakwenda kupotea kutokana na uvunaji usio endelevu.



Wafugaji wa Kimasai wakiwa wameanzisha makazi katikati ya Hifadhi ya Msitu wa Mlima Mbwego katika Kijiji cha Mnkonde kilichoko Kata ya Msanja wilayani Kilindi kinyume cha taratibu.

**HALI YA MISITU YA VIJIJI TANGA**

Kama ilivyo katika maeneo mengi ya nchi yetu, Mkoa wa Tanga una misitu inayomilikiwa na serikali, misitu inayomilikiwa na serikali za vijiji, inayomilikiwa na halmashauri na misitu katika ardhi ya jumla (general land).

Makala hii inajikita zaidi katika kuangalia misitu inayomilikiwa na vijiji ambayo ni takribani asilimia 47 ya misitu yote na kumbukumbu zilizopo zinaonesha kwamba ndiyo iliyo katika hatari ya kutoweka. Mathalani Wilaya ya Kilindi yenye vijiji 102, ni vijiji 36 tu vyenye misitu. Kwa upande wa Wilaya ya Handeni yenye vijiji 91 ni vijiji 18 tu ambavyo bado vina misitu!

Baadhi ya vijiji havina misitu rasmi ingawa ilikuwepo lakini imetoweka kutona na sababu mbalimbali, kubwa zikiwa ni shughuli za binadamu kama kugeuza misitu kuwa mashamba au makazi, kukata miti kwa sababu ya mkaa, kuni na mbao kwa njia isiyo endelevu, kuchoma moto na uchungaji mifugo.

Sheria ya Misitu Na. 14 ya 2002, inavipa vijiji mamlaka ya kumiliki, kusimamia na kutumia raslimali za misitu kwa asilimia 100 kupitia Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (CBFM).



Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi katika Kijiji cha Lusane kilichoko Kata ya Tunguli, Wilaya ya Kilindi, Isaya Nyange.



Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Albert Musando: Tutatoa ushirikiano kwa mradi IFBEST kadri utakavyohijitaka

**MRADI WA IFBEST NINI?**

Mradi wa IFBEST unaendeshwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa kushirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU), kupitia Wizara ya Fedha ya Tanzania.

Ofisa Utawala na Uraghabishi wa MJUMITA, Elida Fundi anasema mradi huo wa miaka mitatu ulioanza mwaka jana, unalenga vijiji 13 kwenye Wilaya nne za Mkoa wa Tanga; Kilindi, Pangani na Mkinga. Hata hivyo, anasema wameanza na vijiji vinane.



Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Hashim Mgandilwa

Katika mradi huo, Elida anasema vijiji huwezeshwa kufanya matumizi bora ya ardhi, wanavijiji, hupewa elimu ya uhifadhi na kulinda mazingira yao kwa maana ya kufanya ulinzi shirikishi wa misitu (CBFM), elimu juu ya uvunaji endelevu wa misitu, elimu ya utawala bora, elimu kuhusu vyama vya kuweka, kukopa na elimu kuhusu masuala ya jinsi na ujinsia. Mradi pia unazijengea uwezo halmashauri na wadau mbalimbali zikiwemo taasisi za kiraia kuhusu masuala ya usimamizi shirikishi wa misitu.

Anasema mbali na kuona vijiji vinanufaika na mazao ya misitu kupitia uvunaji endelevu, mradi pia unawawezesha wananchi kufanya shughuli nyingine za uzalishaji kama biashara na uvunaji asali na vikundi vya kuweka na kukopa badala ya kutegemea mazao ya misitu na hasa uvunaji wa kuni na mkaa.

Ofisa Mradi wa IFBEST Wilaya ya Kilindi, Peter Mtoro, anasema kijiji kikishapokea mradi, kinapimwa ili kujua mipaka na kisha kinapanga matumizi bora ya ardhi ambapo wanatenga eneo la makazi, eneo la msitu, mashamba, malisho na eneo kwa ajili ya kujenga taasisi za kijamii kama shule.

Anasema kijiji huunda kamati mbalimbali ikiwemo ya maliasili ambayo ina jukumu pia la kufanya doria msituni mara kwa mara.

Ofisa Mradi wa IFBEST katika vijiji vya Handeni, Augustine Gervas anazidi kufafanua kwamba msitu ukishatengwa, eneo la msitu hutengwa tena kwa ajili ya uzalishaji wa mbao au mkaa.

"Kwa mfano, msitu wa hifadhi wa kijiji cha Gendagenda, katika kata ya Mgambo una ukubwa wa hekta 4779.5 lakini ni asilimia 16 tu ya msitu (hekta 800) zilizotengwa kwa ajili ya uzalishaji mkaa kwa njia



Ofisa Utawala na Uraghabishi wa Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), Elida Fundi (wa pili kulia) akiwa na baadhi ya viongozi akina mama katika mradi wa kuleta Suluhisho la Ujumuishaji wa Misitu na Nishati Endelevu ya Tungamotaka Tanzania (IFBEST) katika kijiji cha Lusane, Wilaya ya Kilindi, Tanga.



Eneo la ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Mlima Mbwego, katika Kijiji cha Mnkonde kilichoko Kata ya Msanja, wilayani Kilindi, Tanga likiwa limevamiwa na mtu aliyegeuza kuwa shamba

endelevu miaka yote,” anasema.

Anasema katika asilimia hiyo 16 kunatengwa vitalu ambavyo mkaa huvunwa kwa rukaruka. Kwamba kikivunwa kitalu A, kitalu B kinarukwa na ambacho kitavunwa baada ya miaka 21 wakati ambapo wakati huo kitalu A kitakuwa kimeshageuka kuwa msitu tena.

“Tunawafundisha pia wanakijiji kufanya tanuri kichugu ambalo hutoa mkaa mwingi na madhubuti na ambao hautoi moshi,” anasema.

**MGOGORO ULIODUMU MIAKA 22**

Wakazi wa Kijiji cha Lusane wanashukuru ujio wa mradi huo sambamba na juhudi za Mkuu wa Wilaya, Hashim Mgandilwa katika kuwasaidia kumaliza mgogoro wa ardhi kati yao na kijiji jirani cha Kitingi uliodumu kwa takribani miaka 22.

Mtendaji wa Kijiji cha Lusane, Mbaraka Mazige anasema moja ya faida ambayo wameiona kwenye kijiji chake ni kumaliza mgogoro huo.

“Tunashukuru pia Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Hashim Mgandilwa kuingilia kati tatizo la mipaka kwani pia alitumia muda wake mwingi kuja kusuluhisha huu mgogoro ambao ulikuwa unatishia amani,” anasema.

Anasema hatua hiyo ilifikiwa baada ya eneo la mipaka ya kijiji kupimwa na ndipo kukawa na makubaliano ya kuweka mipaka ipasavyo na vijiji vya jirani.

Mwenyekiti wa Wafugaji wa Kata ya Tunguli ambaye ni mkazi wa kijiji hicho cha Lusane, Parakole Leteto anafafanua kwamba wakati wa mgogoro wao, mtu angeweza kuamka akakuta njia ambazo mifugo inapita kwenda malishoni au mnadani imegeuzwa shamba!

“Sasa utaona hapo mtu akipitisha mifugo atadaiwa amepita kwenye shamba la mtu na atapigwa faini. Lakini aliyelima kwenye njia ya mifugo haonekani kama anakosa. Tunashukuru sasa suala kama hilo halitokei tena,” anasema.

Mchungaji wa Kanisa la Baptisti ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Ardhi la kijiji hicho, Isaya Nyange anasema baada ya kijiji kuwa na matumizi bora ya ardhi sasa kila mmoja anajua ni eneo gani afanye nini.

“Zamani mambo yalikuwa holela na tulikuwa hatujui. Lakini sasa tuna eneo la malisho, eneo la makazi, eneo la mashamba na eneo la msitu kwa hiyo tuna mpango mzuri wa matumizi ya ardhi yetu,” anasema.

Anasema wametunga pia sheria ndogo za halmashauri ya kijiji ambapo mtu akikutwa anavuna raslimali za misitu bila kufuata utaratibu au analima sehemu ya makazi anapigwa faini.

Mkuu wa Maendeleo ya Ardhi wa Halmashauri ya Kilindi, Natus Manumbu, anasema migogoro ya mipaka huleta uhasama baina ya kijiji na kijiji huku kukosekana kwa matumizi bora ya ardhi kukisababisha migogoro ya ndani ya kijiji.

Anasema wangetamani kupima mipaka ya vijiji vyote vya Wilaya ya Kilindi vipatavyo 102 na hivyo kuvifanya viwe na matumizi bora ya ardhi lakini wanashindwa kufanya hivyo kutokana na ufinyu wa bajeti.

“Ndio maana utaona mpaka sasa ni vijiji 15 tu ndivyo vyenye matumizi bora ya ardhi katika wilaya yetu. Ndio maana mashirika yasiyo ya kiserikali kama TFCG na MJUMITA yanapotuletea miradi kama hii tunawashukuru sana.”

Kuhusu mgogoro wa mipaka baina ya kijiji cha Lusane na Kitingi, Manumbu anasema baada ya suluhu kupatikana, ramani mpya ya mipaka ya vijiji hivyo imeshaandaliwa na kinachosubiriwa ni ramani hiyo kusajiliwa.

**FAIDA ZA KIUCHUMI**

Mwenyekiti aliyemaliza muda wake katika Kijiji cha Mnkonde kilichoko katika Kata ya Msanja, Juma Kihala, anasema walianza kupata elimu kuhusu umuhimu wa kuhifadhi misitu kupitia mradi wa FORVAC, na sasa wanaendelea na uhifadhi kupitia mradi wa kuleta Suluhisho la Ujumuishaji wa Misitu na Nishati Endelevu ya Tungamotaka Tanzania (IFBEST).

Anasema hapo awali msitu wa kijiji ulikuwa unavunwa kiholela, lakini baada ya kuanzisha ulinzi shirikishi na uvunaji endelevu, kijiji kimepata fedha zilizowezesha kukamilisha ujenzi wa zahanati kwa kununua madirisha 16 ya aluminium, kuchangia ujenzi wa msikiti, na kisima cha maji.

Kwa upande wa kijiji cha Maswaki kilichoko Kata hiyo ya Msanja ambacho pia kinatekeleza mradi huo, aliyekuwa mwenyekiti wa kijiji hicho, Kilo Hussein anasema vijana katika kijiji chake wamepata elimu ya kuzalisha mkaa na mbao kwa njia endelevu na hivyo wako mbioni kuanza kuzalisha mkaa na anaamini sasa kijiji kitaanza kupata faida kwani huko nyuma msitu wao ulikuwa ikivunwa kiholela na ulikuwa unakaribia kupotea.

**KWANINI MKAA?**

Ofisa wa Udhibiti na Tathmini kutoka TFCG, Eward Emily anasema pamoja na serikali kuhimiza kujitenga na matumizi ya nishati isiyo salama ya kuni na mkaa, huenda ikachukua miaka kadhaa kufikia hatua hiyo.

Anasema katika kipindi hiki cha kuelekea asilimia 80 ya wanaotumia nishati safi ifikapo 2034, bado mkaa utakuwa unaendelea kutumika na hivyo ni muhimu uzalishaji katika kipindi hiki ukawa unafanyika kwa njia endelevu ili kulinda misitu kuliko kuacha.

**KUUZA HEWA UKAA**

Takribani wilaya zote mkoanibTanga zinajipanga kuanza kuuza hewa ukaa na hivyo mradi wa IFBEST unaoimarisha utunzaji wa misitu ni hatua muhimu kuelekea kwenye hatua hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Albert Musando anasema wilaya yake ilipeleka madiwani katika Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi ili kuona na kujifunza wanavyonufaika na kuuza hewa ukaa.

Diwani wa Kata ya Mgambo, Hamisi Mwangona ambaye ni miongoni mwa waliokwenda Katavi anasema walijionea namna ambavyo vijiji katika wilaya hiyo vinajenga huduma za kijamii kama shule, zahanati au kuchimba visima kutokana na kuuza hewa ukaa.

“Ndio maana tunapambana kuhakikisha msitu wa Gendagenda unasimama ili mbali na kutupa manufaa ya kuuvuna kwa njia endelevu lakini na sisi pia tuvune fedha kwa kuuza hewa ukaa,” anasema.

Kuuza hewa ukaa ni mchakato wa kuuza “mikopo ya kaboni” ili kufidia utoaji wa gesi chafu. Makampuni au watu hulipa kwa miradi inayopunguza hewa chafu, kama kusimamia misitu na upandaji miti ili kufikia malengo ya mazingira safi. Miti inachukuliwa kama mapafu ya kunyonya hewa ukaa, hususani inayozalishwa na viwanda katika nchi zilizoendelea na ambavyo ndivyo hutoa fedha hizo.

**VICOBA NA SAUTI YA MWANAMKE**

Kwa kuwa moja ya vipengele vya mradi ni elimu juu ya utawala bora, elimu ya ushirika wa kuweka na kukopa na elimu kuhusu jinsi na ujinsia, wanawake katika vijiji vya mradi wamenufaika sana na hali hiyo.

Mradi umewawezesha kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa (VICOBA), na pia kuwajengeza wa kuzungumza mbele ya wanaume na kugombea uongozi.

Lucia Zuberi, mama wa Kimasai kutoka Kijiji cha Lusane, anasema kupitia mradi huo wameanzisha vikundi viwili vya kuweka na kukopa, kila kimoja kikiwa na wanachama 30. Pia anasema kila kikundi huwa na mfuko wa dharura ambao unamwezesha mwanachama kukopa wakati wowote na kulipa taratibu.

“Mimi niko kwenye kikundi cha Sinyata. Tulianza kikundi hivi karibuni tu (Julai), lakini tumeshafikisha shilingi 1,400,000. Majuzi tumekopeshana shilingi 900,000 na wengi wetu tumeanzisha biashara ndogondogo,” anasema.

Mariam Parikole wa kikundi cha Eroto anasema mradi umewasaidia wanawake kupata nafasi ya kuzungumza mbele ya wanaume, kugombea uongozi na kufanya biashara bila bughudha.

“Kabla ya mradi, sisi wanawake wa Kimasai tulikuwa nyuma kabisa. Hatukuwa na kauli mbele ya wanaume, lakini sasa tunakwenda sambamba na tumo kwenye uongozi wa kijiji,” anasema mama huyo ambaye pia ni mjumbe wa Kamati ya Maliasili ya kijiji.

Sofia Madeni wa Kijiji cha Mnkonde, Kilindi, ambaye hapo awali alikuwa akiuza kuni kujikimu, kupitia VICOBA sasa anajishughulisha na kuuza mbogamboga. Lucia Msongela kutoka kijiji hicho anasema hivi karibuni alikopa shilingi 500,000 kutoka kwa kikundi chao cha VICOBA ili kuboresha biashara yake ya vitenge na kulipa ada za shule za mwanawe.

**CHANGAMOTO**

Moja ya changamoto kubwa ni misitu inayohifadhiwa kuendelea kuvamiwa pale ulinzi shirikishi unapolegalega.

Mathalani, wananchi wa Kijiji cha Mnkonde, Kata ya Msanja wilayani Kilindi, wameomba mamlaka husika kuwaondoa wafugaji wa jamii ya Kimasai walioweka makazi kwenye hifadhi ya msitu wa kijiji hicho ya Mlima Mbwego.

Mwenyekiti aliyemaliza muda wake kijijini hapo, Juma Kihala, anasema wafugaji hao wamejenga makazi katika msitu wa kijiji na taratibu za kuwaondoa zimekuwa ngumu.

Mmoja wa wazee wa kijiji hicho, Zuberi Madeni, anasema uwepo wa makazi ya watu katika msitu huo umesababisha pia shughuli za ufugaji nyuki waliokuwa wakifanya katika msitu huo kutoenda vizuri, akidai kwamba mizinga inaibiwa na kuharibiwa.

Madeni anasema tatizo la wafugaji ni kuingia kijijini bila kupitia taratibu za kujitambulisha na kusaidiwa makazi na viongozi husika.

Mmoja wa viongozi wa Kamati ya Mazingira ya kijiji hicho, Zubeda Kihiyo, anasema kuwa Kijiji chao kina mpango wa matumizi bora ya ardhi, ambapo kuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya makazi na malisho, lakini wafugaji wamekuwa hawafuati utaratibu.

Waandishi wa habari walipozuru msitu huo walikuta eneo likiandaliwa kwa ajili ya kilimo.

Afisa Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira wa Halmashauri ya Kilindi, Adam Sylvester, anasema tatizo hilo wanalijua na wanalishughulikia.

**KAULI ZA VIONGOZI**

Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Mazingira, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Napoleon Mlowe anasema kwa sababu mradi wa IFBEST una manufaa mengi, wameanza kutenga fedha ili kuambukiza elimu hiyo kwa vijiji vingine. “Tayari tumetenga shilingi milioni 16 kwa ajili hiyo.”

Mkuu wa Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, Hashim Mgandilwa analishukuru Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kwa kuanzisha mradi wa uhifadhi katika vijiji vitano wilayani humo na hivyo kusaidia misitu ya vijiji hivyo kubaki salama.

Anaupongeza pia Umoja wa Ulaya (EU) kwa kufadhili mradi huo kupitia Wizara ya Fedha ya Tanzania.

“Tunaheshimu mchango wenu (TFCG na MJUMITA). Ingawa uharibifu wa mazingira katika wilaya yetu si mkubwa sana lakini lazima tulinde maeneo yetu. Ujio wenu utasaidia sana maeneo yetu kubaki salama... Na kwa kweli ni lazima tuhifadhi mazingira yetu kwa sababu ukiyachezea (mazingira) yatakuadhibu,” anasema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, Crispin Mng’anya, akizungumza kwa niaba ya mkurugenzi wa halmashauri hiyo amewaomba TFCG na MJUMITA kuona uwezekano wa kuongeza idadi ya vijiji wanavyohudumia katika wilaya hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Musando pia anapongeza uwepo wa mradi wa IFBEST katika wilaya yake na kuahidi kutoa ushirikiano wowote utakaohitajika.

Shabani Mruma, akizungumza kwa niaba ya Kaimu Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Tanga, ameushukuru Umoja wa Ulaya kwa kufadhili wa mradi wa IFBEST umbao umesaidia kutatua migogoro ya ardhi kutoka na kuanzisha mipango ya matumizi ya ardhi, hatua ambayo inawezesha kufanya kila kipande cha ardhi kujulikana matumizi yake.

“Ninashauri halmashauri zetu kila mwaka zitenge fedha kwa ajili ya kupanga matumizi bora ya ardhi,” anasema.



# Uchaguzi Botswana na uwezekano wa chama tawala kushinda

LEO, wananchi wa Botswana wanafanya uchaguzi mkuu ambapo Rais Mokgweetsi Masisi, anashindana na wagombea wengine watatu wakubwa akitafuta muhula wa pili kwenye taifa hilo lenye utajiri mkubwa wa almasi.

Wagombea wengine ni Duma Boko wa Umbrella for Democratic Change (UDC), Dumelang Saleshando wa Botswana Congress Party (BCP) ambacho kilijitoa kutoka kwenye muungano wa UDC na Mephato Reatile wa chama cha Botswana Patriotic Front (BPF).

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, uchaguzi huo huenda ukawa na ushindani mkali kulingana na wachambuzi ingawa upinzani uliogawanyika unatoa nafasi kubwa kwa chama tawala cha Masisi, cha Botswana Democratic Party (BDP) kushinda. Chama hiki kimetawala taifa hilo la watu milioni 2.3 tangu kujipatia uhuru wake kutoka kwa Uingereza mwaka 1966.

Botswana imekuwa na ustawi na uchumi mzuri kwa muda mrefu kutokana na utajiri wa almasi, pamoja na idadi ndogo ya watu ambao hupewa huduma bure za elimu na afya.

Hata hivyo, kushuka kwa bei ya almasi kwenye soko la kimataifa katika miaka ya karibuni kumepelekea kushuka kwa mapato ya ndani na kuyumbisha uchumi, na hivyo taifa hili linajielekeza kwenye kuwekeza kwenye sekta nyingine.

Wapinzani wanasema kuwa chama cha BDP, kimebaki madarakani kwa muda mrefu zaidi na kwa hivyo wanakinyooshea kidole kwa kuvuruga uchumi pamoja na ufisadi, madai ambayo BDP inayanusha.

Wakati wa mdahalo uliofanyika wiki iliopita, Masisi alisema kuwa ni kweli almasi zinazozalishwa nchimo humo hazijanunuliwa tangu Aprili, na kwamba uchumi umeshuka, lakini akasema mfumo wa uchumi ungali thabiti.

Katika ilani yake, BDP kinahimiza kuna na mabadiliko. "Hebu tubadilishe nchi yetu kwa pamoja na kujenga ustawi kwa wote," Rais Mokgweetsi Masisi ambaye ameongoza nchi hiyo tangu 2018 anasema akimaanisha kwamba nchi inahitaji mabadiliko.

Ingawa wachambuzi wanasema matokeo ya uchaguzi ni magumu kutabirika wakati huu, lakini BDP inaonekana kuendelea kuungwa mkono na wengi na kimekuwa kikipata wingi mzuri wa viti vya wabunge katika chaguzi 11 tangu uhuru mwaka 1966.

BDP imekuwa ikisifiwa kwa kusimamia mabadiliko makubwa na ya amani kutoka nchi maskini, yenye kilomita chache za barabara zilizojengwa kwa lami wakati wa uhuru, hadi kuwa nchi yenye viwango vya juu vya maisha barani Afrika na uchumi mzuri huki ikiwa na miundombinu ya barabara imara.

Msingi wa mabadiliko haya ni hifadhi kubwa ya almasi ya na uongozi makini katika kusimamia raslimali hizo. Botswana ndiyo nchi inayozalisha almasi kwa wingi zaidi duniani.

Hata hivyo, kwa sasa Botswana inakabiliwa na changamoto kubwa za kiuchumi na ndiyo maana Rais Masisi sasa anazungumzia mabadiliko. Takwimu zinaonesha kwamba mtu mmoja au zaidi kati ya watu wanne hana ajira, huku idadi kubwa wakiwa vijana, kwa mujibu wa Benki ya Dunia.

Profesa wa siasa katika Chuo Kikuu cha Botswana, Zibani Maundeni, anaueleza uchumi huu kama "uchumi usio na ajira."

"Tunatoa wahitimu kila mwaka lakini uchumi hauzalishi ajira za kutosha kwa ajili yao," anasema.

Aidha inasemwa kwamba hata utajiri wa Botswana unaotamkwa haujasambaa sawasawa kwa watu wake milioni 2.3 kwa maana ya kwamba matajiri na watu wenye uchumi wa kati ni wachache kulinganisha na maskini kwa mujibu wa kipimo kinachoitwa Gini index.

Sekta ya almasi sasa nayo si ya kutegemewa sana kama ilivyokuwa miaka ya nyuma kutokana na mahitaji yake kuendelea kushuka.

Hata hivyo, Masisi na chama chake tawala wanaendelea kuonesha kujiamini kuhusu kuboresha uchumi wa nchi hiyo.

Katika mkutano wa kampeni kwenye ngome ya upinzani katikati ya Botswana, Rais aliwasili kwa mtindo akitumia gari la umeme lililotengenezwa nchini humo.

Akitelemka kwenye gari hilo, mwalimu huyo wa zamani mwenye umri wa miaka 63 alicheza kuelekea jukwaani akiwasalimu wafuasi wake waliovalia rangi za chama; nyekundu na nyeupe.

Eneo hilo ambalo ni karibu na makazi ya rais wa zamani, Ian Khama, lilichagua wabunge watatu wa upinzani mwaka 2019 baada ya Khama kujitenga na BDP na kusaidia kuanzisha chama cha Botswana Patriotic Front (BPF), akisema alijuta kumteua Masisi kama mrithi wake.

Mvutano mkubwa kati ya wawili hao ulisababisha Khama kuondoka nchini, akidai kuwa serikali ilijaribu kumuua kwa sumu. Khama alishtakiwa kwa utakatishaji fedha na makosa mengine, ambayo yote anayakana.

Hali hiyo pia ilimaliza ushawishi wa kisiasa wa familia yake - baba yake, Sir Seretse Khama, aliyekuwa rais wa kwanza wa nchi hiyo na alihudumu kwa miaka 14 kuanzia mwaka 1966.

"Samahani, tafadhali rudini nyumbani na pia muwalete wengine," Masisi alisema kwenye mkutano huo akiwahimiza wapiga kura kurudi waliokihama chama hicho kurejea. Mmiliki wa saluni ya nywele, Thandiwe Potso, mwenye umri wa miaka 32, alionekana kuridhika. "Masisi anaelewa changamoto zetu na ameleta programu bora za kufadhili biashara zetu."

Kabelo Selemo, mwenye umri wa miaka 45, anakubaliana naye akisema; "Sera zake zimetusaidia kukua; kama unavyoona, hatuagizi mboga tena. Ninaamini katika maono yake kwa ajili ya siku zetu zijazo."

Lakini kwa mujibu wa kura ya maoni, Baadhi ya raia wa Botswana si rahisi kuwashawishi. Shirika la utafiti lisiloegemea upande wowote la Afrobarometer, lilitoa ripoti ya kura za maoni ambayo si rafiki sana kwa chama tawala. Lilisema kuwa licha ya nchi hiyo kuwa miongoni mwa zinazoongoza kwa utawala bora barani Afrika, watu wa Botswana walikuwa na mtazamo kwamba viongozi wengi serikalini wanajihusisha na vitendo vya ufisadi.

Hata hivyo, Msemaji wa BDP, Kagelelo Banks Kentse, alihoji uhalali wa kura hiyo akisema Afrobarometer imekuwa ikitumiwa vibaya na wapinzani wa chama hicho na alitarajia kwamba haitatoa matokeo yenye kuunga mkono chama tawala licha ya juhudi ambazo chama hicho kinafanya katika kuwaletea maendeleo wananchi.

"Itakuwa ni makosa kusema kwamba tunaamini kwa asilimia 100 kuwa tutashinda," Kentse aliiambia BBC. Alikiri kuwa kiwango cha ukosefu wa ajira hakileti picha nzuri, lakini akasema kuwa kila taifa barani Afrika linakabiliwa na changamoto kama hizo, akiongeza kuwa chama chake kinatoa ahadi ya kuunda ajira 300,000 zaidi.

Lakini kiongozi wa moja ya vyama vikubwa vya upinzani, Dumelang Saleshando, anasema serikali ya sasa imepora na kuiga mawazo na sera za wengine kikiwemo chama chao.

Anasema kuwa chama chake cha Botswana Congress Party (BCP) kilikuwa cha kwanza kuweka mkakati wa ajira na sasa BDP inakwenda mulemule. Moja ya kaulimbiu za Saleshando ni: "Okoa Botswana."

"Nadhani watu wameiona BDP ilivyo," anasema. "Haiwezi kudai kuwa ni chombo cha mabadiliko. Yenyewe imekuwa ikiwa na sera ya kudumisha utulivu bila kufikiria mustakabali wa hali ya wananchi hususani ukosefu wa ajira. Sasa kwa hofu ya kupoteza kura wanajaribu kuhubiri kile ambacho hawaamini."

Wafuasi wa chama kingine cha upinzani - Umbrella for Democratic Change (UDC), ambacho kilishika nafasi ya pili katika uchaguzi wa mwaka 2019, wamekuwa pia wakijitokeza kwenye kampeni hususani kaskazini mwa mji mkuu, Gaborone.

Wakiwa wamevaa fulana za bluu na kofia (kapelo), katika kampeni za mwishomwosho walimshangilia sana kiongozi wao, Duma Boko. Yeye amekuwa akidai kwamba Watswana wanateseka bila sababu chini ya BDP akitaka watu wakipigie kura chama chake. Alikuja na madai mengine kwamba kuna majaribio ya kuiba kura.

"Nawaomba nyote kuwa waangalifu na baada ya kupiga kura ili kuiondoa BDP mkae kwenye kituo cha kupiga kura kulinda kura zenu," alisema.

Thapelo Dimpe, mwalimu wa zamani mwenye umri wa miaka 45, anatamani kuona chama tawala kikishindwa. "Masisi ametukatisha tamaa kuhusu mageuzi ya elimu. UDC inataka kuwekeza katika shule zetu na kuwawezesha vijana wetu kwa elimu wanayostahili," anasema.

Tusubiri kuona mwisho wa haya leo!



# Mvutano ni mkali baina ya Trump na Kamala

ZIMEBAKIA takribani siku sita tu kuanzia leo Wamerekani waingie katika uchaguzi wa urais kwa mwaka 2024. Uchaguzi huo unafanyika Jumanne ijayo Novemba 5. Uchaguzi huo ni kati ya mgombea wa chama cha Republican, Donald Trump na Kamala Harris wa Democratic.

Kampeni za mwaka huu zimekuwa za kuvutia kwa kuwa na mjadala mkubwa kuhusu masuala ya kiuchumi, haki za kijamii, na ushawishi wa sura maarufu kama vile Michelle Obama na wanamuziki maarufu wanaowaunga mkono wagombea.

### KAMPENI ZA KAMALA HARRIS

Kamala Harris ameangazia masuala ya kijamii, akisisitiza haki za wanawake, upatikanaji wa huduma za afya kwa wote, na usawa wa kijinsia. Harris pia anajikita kwenye haki za kijamii, hasa kwa jamii zilizotengwa.

Sera zake za kijamii zinalenga kuongeza upatikanaji wa huduma za afya na elimu, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya juu kwa gharama nafuu, ambayo inakusudiwa kusaidia familia zenye kipato cha chini. Ameahidi pia kutetea haki ya utoaji mimba, suala linalozua hisia kali kati ya wafuasi wake na wapinzani wake.

Kiuchumi, Harris anapendekeza kuongeza ushuru kwa matajiri na kuimarisha miradi ya kijamii ili kufikia usawa wa kiuchumi na kupunguza gharama za maisha. Sera hii inalenga pia kuimarisha sekta ya afya kwa kupunguza gharama za bima ya afya na kuongeza misaada kwa wale wenye kipato cha chini.

Katika kampeni zake, Harris anapata uungwaji mkono kutoka kwa wasanii na wanamuziki wa chama Democratic, kama vile Taylor Swift, ambaye amekuwa akiwasihi mashabiki wake kujitokeza kwa wingi kwenye uchaguzi ili "kusimamisha uharibifu wa demokrasia."

Wanamuziki wengine maarufu kama Beyonce, pamoja na watendaji wa Hollywood, wanamsaidia Harris kwa kuwaonesha mashabiki wao umuhimu wa kushiriki kikamilifu katika uchaguzi huu.

### KAMPENI ZA DONALD TRUMP

Donald Trump, kwa upande wake, amejikita zaidi katika masuala ya uchumi na usalama wa ndani, akiahidi kupunguza ushuru, kudhibiti uhamiaji usio halali, na kuimarisha sera za "Amerika Kwanza."

Anadai kwamba sera hizi zitarejesha nafasi za ajira kwa Wamarekani na kupunguza utegemezi kwa bidhaa kutoka nje. Trump pia ameahidi kupambana na kile anachokiita "ufisadi wa kisiasa" huku akijitolea kuimarisha haki za kijamii kwa njia zake mwenyewe, hasa kwa jamii za vijijini na maeneo yenye wapiga kura wa kizungu.

Trump amepata uungwaji mkono kutoka kwa wanamuziki wa mtindo wa country na baadhi ya nyota wa zamani wa muziki, ambao wanahamasisha wafuasi wao kuunga mkono msimamo wake wa kitaifa na kiuchumi.

Wasanii kama Kid Rock na Ted Nugent wamekuwa wakiunga mkono hadharani kampeni ya Trump, wakieleza kuwa wameridhishwa na malengo yake ya "kuweka Amerika mbele."

### MICHELLE OBAMA

Ingawa si mgombea rasmi, Michelle Obama amekuwa na ushawishi mkubwa katika kampeni za uchaguzi kwa kumuunga mkono Harris na kluwataka wafuasi wa democrati n ahata Republican kumchagua Harris. Michelle, ambaye ni maarufu sana kipenzi cha vijana na wanawake, amekuwa akihamasisha watu kushiriki kikamilifu kwenye uchaguzi.

Kwenye mikutano yake ya hadhara, Michelle amekuwa akihimiza umoja wa kitaifa na umuhimu wa kudumisha misingi ya demokrasia ya Marekani. Anaamini kuwa uongozi unaoheshimu haki za raia na usawa wa kijamii ni muhimu kwa mustakabali wa taifa hilo.

Michelle Obama anaungwa mkono na wasanii wengi wa kizazi kipya na wa zamani, wakijitokeza kwenye mitandao ya kijamii ili kuhamasisha wafuasi wao kujiandikisha kupiga kura na kuunga mkono demokrasia.

Nyota wa muziki kama Beyoncé na Billie Eilish, ambao wamekuwa mstari wa mbele kuunga mkono demokrasia, wanatumia ushawishi wao kuhamasisha vijana kushiriki kikamilifu katika uchaguzi huu muhimu.

### HALI YA KURA ZA MAONI

Kura za maoni zinaonesha kuwa Kamala Harris anaongoza kwa tofauti ndogo dhidi ya Trump katika ngazi ya kitaifa. Hata hivyo, ushindani unazidi kuongezeka katika baadhi ya majimbo muhimu kama Pennsylvania na Georgia, ambapo wapiga kura wa maeneo hayo bado hawajaamua vizuri ni nani wanayemuunga mkono. Kura hizi zinaonyesha kuwa uchaguzi huu una nafasi kubwa ya kuwa na ushindani mkali hadi dakika ya mwisho

Kimsingi Harris anaungwa mkono zaidi na makundi ya wanawake, vijana, na wapiga kura wa jamii za watu weusi na kutokaAsia. Kwa upande mwingine, Trump anaungwa mkono zaidi na wapiga kura wa maeneo ya vijijini na wapiga kura wa kizungu.

Kwa hiyo Uchaguzi wa 2024 ni moja ya chaguzi zenye ushindani mkubwa katika historia ya Marekani. Kampeni za Trump na Harris, pamoja na ushawishi wa Michelle Obama na wanamuziki maarufu, zinaonesha jinsi kila upande unavyojaribu kushawishi wapiga kura kwa nguvu zote.

Wengi wanaona kuwa uchaguzi huu una umuhimu wa kipekee kwa mustakabali wa Marekani, na unatarajiwa kuwa na athari kubwa kwa masuala ya kiuchumi, kijamii, na kisiasa nchini humo.

### ELECTORAL COLLEGE

Katika uchaguzi wa Marekani, wapiga kura wa kitaifa hushiriki kupiga kura kwa wagombea urais, lakini matokeo ya mwisho hutegemea mfumo wa kipekee unaoitwa "Electoral College," ambapo wawakilishi maalumu kutoka majimbo yote hutoa kura zao rasmi mwezi Desemba ili kuchagua rais baadaya uchaguzi wa kitaifa.

Mfumo huu uliwekwa na waasisi wa taifa ili kutoa usawa kwa majimbo mbalimbali na kuzuia kutawaliwa na majimbo yenye idadi kubwa ya watu pekee.

### JINSI ELECTORAL COLLEGE INAVYOFANYA KAZI

Kila jimbo lina idadi maalumu ya elekto (electors0 inayolingana na jumla ya wawakilishi wake katika Bunge la Wawakilishi (Congress) na Seneti. Kwa jumla, kuna kura za "electors" 538, na mgombea urais anayepata kura 270 au zaidi ndiye anayeshinda uchaguzi.

Mara baada ya uchaguzi wa kitaifa kufanyika mnamo mwezi Novemba, wapiga kura wanachagua mgombea wao, lakini kura hizi zinahesabiwa kama mapendeleo ya jimbo. Katika majimbo mengi, mshindi wa kura nyingi jimboni hupata kura zote za "electors" za jimbo hilo. Hata hivyo, Maine na Nebraska hutumia mfumo wa kugawanya kura hizo kulingana na ushindi wa maeneo ya bunge na kura za kitaifa jimboni.

### MFUMO WA MAJIMBO MUHIMU (SWING STATES)

Majimbo yanayobadilika mara kwa mara upande wa kisiasa, kama Pennsylvania, Florida, na Wisconsin, yana umuhimu mkubwa katika uchaguzi. Majimbo haya yanaweza kuathiri matokeo ya mwisho kwa sababu yana idadi ya kutosha ya kura za "electors" ambazo zinaweza kuamua mshindi wa mwisho.

Mfumo huu wa Electoral College umeleta mjadala mkubwa nchini Marekani kwa sababu wapiga kura katika majimbo yenye watu wachache au yenye msimamo wa upande mmoja mara nyingi wanahisi kuwa kura zao hazina uzito mkubwa. Wengine wanahoji kuwa mfumo huu ni wa muhimu katika kulinda sauti ya majimbo yote na kwamba unazuia mgombea kushinda urais kwa kutegemea tu kura za majimbo makubwa.



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Miaka 20 ya Bodi ya Mikopo kutimiza ndoto za vijana



Juma, kijana kutoka kijiji cha Kurwaki, Musoma vijijini anasema alikabiliwa na changamoto nyingi za kifedha katika safari yake ya elimu kutokana na kutoka katika familia maskini. Baba yake (sasa marehemu) alikuwa mkulima na mama yake akiwa mama wa nyumbani

"Nilisoma kwa shida wakati mwingine nikisaidiwa na watu baki. Wakati mwingine, hasa siku za wikiendi au mapumziko, nililazimika kujihusisha na shughuli za uvuvi Ziwa Victiori hadi nilipohitimu kidato cha sita," anasema.

Anasema ngoma sasa ilikuwa namna ya kwenda chuo kikuu baada ya kufaulu kwa ajili ya kusomea ualimu. Juma ambaye kwa sasa ni mwalimu na anajiandaa kurudi kusoma shahada ya pili, anasema ndoto zake za kutinga chuo kikuu zilitimia kutokana na mkopo wa elimu kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

"Nisema tu kwamba bila mkopo nisingekuwa hapa nilipo. Sana sana, nadhani, ningekuwa kijiji nikijihusisha na kilimo au uvuvi. Lakini kwa kutumia elimu yangu nimeboresha pia shughuli za kilimo kijijini ambazo sasa zinaendeshwa na mama kisasa kidogo lakini pia ninamudu kusomesha wadogo zangu wawili," anasema.

Juma ni mmoja wa maelfu ya vijana wa Kitanzania ambao pengine bila uwepo wa Bodi ya Mikopo, ndoto zao za kupata elimu ya juu zisingefanikiwa kabisa kutokana na uwezo mdogo wa kifedha walio nao wazazi wao.

### BODI YA MIKOPO

Ingawa mikopo kwa ajili ya elimu ya juu ilianza kutolewa miaka ya katikati mwa 1990, Bodi ya Mikopo ilianzishwa rasmi mwaka 2004 na kulazimika kuksanya pia madeni ya wanufaika wa nyuma. Kwa mantiki hiyo mwaka huu Bodi imetimiza miaka 20 tangu kuanzishwa kwake.

Kwa kutambua elimu ni ghali na kwa kutambua umuhimu wa elimu ya juu katika jitihada za nchi yetu kupata wataalamu na hivyo kusukuma maendeleo kuanzia mtu binafsi, familia, jamii na taifa kwa ujumla, serikali iliona haja ya kuanzisha bodi hii.

HESLB pamoja na majukumu mengine waliyonayo, wanawajibika zaidi katika kutoa mikopo kwa waombaji wenye sifa stahiki pamoja na kusimamia urejeshaji wa mikopo hiyo ili kuwezesha Watanzania wengi zaidi kupata mikopo hiyo wamudu gharama za elimu wawapo vyuoni.

Gharama hizi ni pamoja na ada, chakula, malazi, udurufishaji wa matini, mafunzo kwa vitendo, vitabu na mahitaji maalumu ya vitivo. Haya yote yanagharimu fedha, ambazo Watanzania walio wengi hawawezi kumudu.

### ELIMU HAINA MBADALA

Methali ya Kiingereza inasema; "Ikiwa unaona elimu ni gharama, basi jaribu ujinga" na kwa hakika ni sahihi kabisa kwani elimu ni gharama lakini ujinga ni janga. Hebu fumba macho na jaribu kufikiria endapo nchi yetu ingekuwa haina wataalamu kama madaktari bingwa, waalimu, wauguzi, wanasheria, wahandisi, maofisa kilimo na kadhalika na kadhalika bila kusahau viongozi wa kisiasa, hali ingekuwaje?

Kwa kufipi, faida za elimu ya juu katika nchi ni pamoja na kuongeza uzalishaji na ubunifu katika sekta mbalimbali na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi na ajira. Ouia kpata viongozi wenye weledi, wanaoweza kusimamia rasilimali za nchi kwa ufanisi na kuimarisha mifumo ya utawala, kuboresha na kuendeleza teknolojia, ubunifu na utafiti na kuongeza maarifa katika jamii katika kuimarisha afya, elimu, na huduma za kijamii.

Hasara za kukosa wasomi katika nchi nyingi lakini miongoni mwa hizo ni kukosa maendeleo kutokana na kukosa wataalamu wa kutosha wa kuendeleza sekta muhimu, kua na utawala duni sambamba na usimamizi mbovu wa rasilimali za taifa; ubunifu duni na kosefu wa ajira na hivyo kuongeza umaskini.

Kwa kutambua kwamba bado kuna Watanzania wengi maskini na elimu ni urithi usio na mbadala kwa vijana wetu kutokana na faida nilizotaja hapo, serikali inatekeleza Sera ya Elimumsingi Bila Ada kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita ambapo serikali inatoa ruzuku ya uendeshaji. Hili ni jambo adhimu na la kupongezwa sana.

Fedha zinazotolewa na serikali hutumika kuendesha shughuli za utawala, taaluma, michezo, mitihani, ukarabati mdogo, ununuzi wa dawa, vifaa vya maabara na kemikali ili kuwezesha mafunzo kwa vitendo hasa kwa masomo ya sayansi kama vile Fizikia, Kemia na Baiolojia.

Ni katijka mukadha huo, elimu ya kati kwa baadhi ya kozi pamoja na elimu ya juu, serikali kupitia HESLB inatoa mikopo kwa waombaji wenye sifa ili kuweza kumudu gharama mbalimbali kama nilivyoeleza hapo juu.

### FEDHA NYINGI ZIMETOLEWA

HESLB inapoadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwake, takwimu zinaonesha kwamba imeshatoa takribani shilingi trilioni 7.2 kwa waombaji mbalimbali ambao wengi wameshahitimu masomo na sasa wanaendelea na maisha yao, wengine wakiwa na ajira rasmi, zisizo rasmi na baadhi wakiwa hawana kabisa ajira au shughuli za kuwaingizia vipato.

Kwa upande wa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu, katika kipindi cha miaka 20 ya HESLB, inakadiriwa kunafaisha waombaji takribani 754,000.

Hata hivyo, takwimu zilizpo zinaonesha kwamba fedha zilizoiva ili zirejeshwe ni shilingi trilioni 2.1 lakini fedha zilizokusanywa ni takribani shilingi trilioni 1.5 ambazo ni sawa na asilimia 71.

### KUSAKA WADAIWA SUGU

Juni 28, 2024, HESLB ilizindua kampeni ya kusaka wadaiwa sugu iliyopewa jina la "Fichua – Kuwa Hero wa Madogo."

Kampeni hii ni ya kizalendo sana ikiwa na lengo la kuwaomba Watanzania na wananchi kwa ujumla kuwafichua wanufaika wa mikopo ambao wameshahitimu masomo yao, tayari wana vipato halali kutoka katika ajira rasmi na zisizo rasmi lakini bado hawajaanza kurejesha mikopo yao.

Katika uzinduzi wa kampeni hii, Mkurugenzi wa HESLB, Dk. Bill Kiwia alisema: "Kampeni hii inalenga kuwashirikisha wananchi kutimiza jukumu la kizalendo la kuwafichua wadaiwa wa HESLB wenye kipato lakini hawajitokezi na kuanza kurejesha.

"Ili kutoa taarifa za wadaiwa, mwananchi anapaswa kutuma jina la mnufaika, chuo alichosoma, eneo analofanyia kazi, jina la kampuni anayofanyia kazi au anayomiliki na eneo ilipo kampuni hiyo."

Kwa mujibu wa Dk. Kiwia, kampeni hii imekuwa ya mafanikio makubwa kutokana na wananchi wengi kutoa taarifa za wahitimu wanufaika wenye kipato kwa HESLB.

Kwa kuwa moja ya changamoto kubwa inayoikabili HELSB ni baadhi ya wanufaika wake wenye vipato kushindwa kurejesha mikopo ni vyema Watanzania tuisaidie bodi hii muhimu sanma kuwafichua hawa ambao wanaendelea kutolipa deni wakati uwezo wanao.

Hatua ya HESLB kushirikisha wadau wengine kama vile Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Taasisi ya Kuchakata Taarifa za Wakopaji wa Benki ijulikanayo kwa jina la Credit Info Tanzania na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuongeza wigo wa kuwasaka wadaiwa sugu kwa njia za kieletroniki ni jambo la kupongeza pia.

Wadau hawa ni muhimu kwani wote kwa pamoja wanashirikiana na HESLB kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) kuwasaka wadaiwa sugu wenye vipato ambao bado hawajaanza kulipa mikopo yao ili itumike kuwasomesha wadogo zao, hatua itakayoongeza idadi ya wasomi katika nchi.

### KUWENI WAZALENDO, JITOKEZENI

Ni ombi langu kwa wanufaika wote wenye vipato ambao bado hawajaanza kurejesha mikopo yao, kujitokeza kwa hiari ili kuanza kurejesha mikopo. HESLB imeboresha mifumo yake ambapo sasa mnufaika anaweza kulipa mkopo wake popote alipo kwa njia ya simu kupitia namba maalumU ya malipo (control number).

Vilevile, waajiri wanao wajibu wa kutoa taarifa kwa bodi pale wanapoajiri mtu aliyepata mkopo ili kuiwezesha bodi kurejesha fedha hizo muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya elimu katika nchi yetu.

Ikubukwe tu kwamba mwajiri anapaswa kukata asilimia 15 tu ya mshahara wa mwajiriwa ni mnufaika wa mkopo hii, kwa hiyo ukiangalia ni kiasi kodogo sana ambacho hakiwezi kuyumbisha maisha na mipango ya mnufaika.

### KUONGEZA FEDHA ZA MIKOPO

Hakuna ubishi kwamba idadi ya Watanzania inaongezeka, idadi ya vyuo vya kati na vikuu inaongezeka na hivyo pia waombaji wa mikopo wenye sifa inaongezeka mwaka hadi mwaka. Hivyo, ni vyema serikali ikaendelea na utaratibu wake wa kuongeza fedha kila mwaka ili kukidhi mahitaji ya waombaji na hivyo kuwawezesha waombaji wengi kupata mikopo.

Hili likienda sambamba na wanufaika kuwa wazalendo na kulipa madeni yao bila 'kukwepakwepa' ili 'madogo' nao wasome ni jambo jema sana.

*Mwandishi wa makala haya ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*

# Maeneo 6 muhimu ya nyuklia ya Iran



UVUMI unazidi kuongezeka kwamba Israel inapanga kushambulia vituo vya nyuklia vya Iran kulipiza kisasi baada ya Tehran kufanya shambulio kubwa zaidi la kombora kuwahi kuishambulia Israel Oktoba mosi, mwaka huu.

Vituo vya nyuklia vya Iran vimejengwa juu ya ardhi na chini ya ardhi.

### KIWANDA CHA KURUTUBISHA URANIUM CHA NATANZ

Natanz ni eneo kuu la kurutubisha uranium nchini Iran, liko kilomita 250 kusini mwa mji mkuu wa Iran, Tehran.

Lina sehemu mbili: Kiwanda cha Majaribio cha Kurutubisha Mafuta (PFEP) na Kiwanda kikubwa cha Urutubishaji Mafuta (FEP), ambacho ni kituo kikuu katika mpango wa Iran.

Sehemu yake kuu imejengwa chini ya ardhi ili kuilinda kutokana na mashambulizi. FEP kilijengwa kwa ajili ya kurutubisha kwa kiwango kibiashara.

Kituo hicho kinaweza kuhifadhi mitambo 50,000 ya kutenganisha uranium nzito na nyepesi.

Mitambo hiyo iitwayo centrifuge ipo 14,000 katika kituo hicho kwa sasa, takribani 11,000 kati yake ikifanya kazi, kusafisha uranium hadi usafi wa asilimia tano.

Hiyo inaweza kutumika kuzalisha mafuta kwa ajili ya mitambo ya nyuklia.

Chini ya mapatano ya nyuklia ya mwaka 2015 (Joint Comprehensive Plan of Action, JCPOA), Iran ilikubali kupunguza urutubishaji hadi asilimia 3.67, lakini baada ya Marekani kujitoa kwenye makubaliano hayo mwaka 2018, Iran ilianza kurutubisha hadi asilimia 60.

Urutubishaji wa uranium unaohitajika kuunda silaha ya nyuklia ni asilimia 90 au zaidi.

Kituo cha Natanz kimekuwa kikilengwa na mashambulizi ya mtandao na hujuma, ikiwa ni pamoja na virusi vya kompyuta vya Stuxnet, vilivyogunduliwa mwaka 2010 na inaaminika ilikuwa ni operesheni ya pamoja ya Marekani na Israel.

Kulikuwa pia na mlipuko kwenye eneo hilo mwaka 2021, na Iran iliilaumu Israel.

Kituo hicho ndicho kitovu cha mazungumzo ya kimataifa na kinakaguliwa kwa ukaribu na Wakala wa Kimataifa wa Nishati ya Atomiki (IAEA), shirika la Umoja wa Mataifa la kuratibu masuala ya nyuklia.

### KIWANDA CHA KURUTUBISHA MAFUTA CHA FORDOW

Kiwanda cha kurutubisha mafuta cha Fordow ni kituo cha chini ya ardhi cha kurutubisha uranium karibu na Qom, karibu kilomita 160 kusini mwa Tehran.

Kimejengwa ndani kabisa ya mlima, ujenzi wake wa siri ulifichuliwa mwaka 2009, na kuibua wasiwasi wa kimataifa kuhusu nia ya nyuklia ya Iran.

Kinaweza kuhifadhi karibu mitambo 3,000 ya kusafishia uranium, Fordow kinalindwa dhidi ya mashambulizi ya kijeshi.

Chini ya JCPOA 2015, Iran ilikubali kukibadilisha Fordow kuwa kituo cha utafiti na kusitisha urutubishaji wa uranium kwa miaka 15.

Lakini, baada ya Marekani kujiondoa katika makubaliano hayo mwaka 2018, Iran ilianza tena shughuli za kurutubisha, na kufikia uranium safi ya asilimia 20 hadi mwaka 2021.

Novemba, 2022, Iran ilizidisha urutubishaji wake hadi asilimia 60 huko Fordow hatua muhimu kuelekea uwezo wa kiwango cha silaha - na kutangaza mipango ya upanuzi mkubwa wa uwezo wake wa kurutubisha, kulingana na IAEA.

Kufikia 2024, ongezeko la shughuli za urutubishaji huko Fordow na teknolojia ya hali ya juu zinaendelea kutoa changamoto kwa juhudi za kimataifa za kuzuia mpango huo.

IAEA inafuatilia eneo hilo, lakini viwango vya juu vya urutubishaji na uwezo uliopanuliwa vimeongeza mvutano na kutatiza juhudi za kufufua makubaliano ya nyuklia. **Itaendelea wiki ijayo...**





# Utata wa kifo cha JF Kennedy wa Marekani-7

**Simulizi kuhusu utata wa kifo cha Rais wa 35 wa Marekani John Fitzgerald Kennedy aliyeingia ofisini Januari 20, 1961 hadi alipouawa Novemba 22 mwaka 1963 inaendelea. Ikiwa ni miaka 61 imepita tangu kifo hicho, tumeangalia safari yake ya kutembelea Jimbo la Texas akiwa na malengo kadhaa, kubwa likiwa ni kujiimarisha kisiasa katika jimbo hilo baada ya kutofanya vizuri sana katika uchaguzi uliokuwa umemwingiza madarakani. Tumeliagalia jinsi alivyopigwa risasi, akakambizwa hospitali na kisha makamu wake, Lyndon Johnson akawa anatakiwa kutangaza rasmi kifo chake ili kuondoa utata. Mwandishi Wetu, HAMID YASSIN anaendelea kuangalia utata kuhusu mtu anayedaiwa kumuua Rais Kennedy, Lee Harvey Oswald kama ni yeye kweli. Wiki iliyopita alieleza namna ambavyo ni ngumu kwa namna inavyoelezwa na serikali kupitia Warren Commission kwa Oswald kupiga risasi ambayo ilimuua Rais Kennedy.**

Katika sehemu hii anaache kidogo kuangalia eneo la la tukio (Dealey Plaza)ili tuangalie masuala kadhaa ambayo yanaashiria na kuonesha dalili ya nani hasa alihusika na kifo cha KF Kennedy. Huko mbeleni tutarejea tena kujadili mambo kadhaa kuhusu mahali na siku ya tukio pale Dealey Plaza.

### NI NANI ALDHAMIRIA KUONA KENNEDY ANAONDOSHWA?

Kabla ya kujadili chochote kuhusu hili ni vyema kukumbushana kwamba hakuna mtu mwenye uhakika kwa asilimia mia moja kuhusu ni nani ambaye alimuua Kennedy.

Tukio la mauaji yake lilipangwa kwa ustadi mkubwa kiasi kwamba hakuna ushahidi ulio 'conclusive' wa kuwaweka wazi pasina shaka yoyote wauaji wa Kennedy.

Kwa hiyo tunachoweza kukifanya ni kuangalia vidhibiti kadhaa muhimu ambavyo vinaweza kutupa mwanga wa nani hasa alihusika naauaji hayo.

Wako ambao wanashikilia msimamo kwamba Lee Harvey Oswald alitekeleza tukio hili kwa utashi wake binafsi pasipo kushirikiana na mtu yeyote yule.

Na pia wapo ambao kila wanavyojitahidi kulitazama tukio hili bado wanabaki na vitendawili na maswali mengi kiasi kwamba inakuwa ngumu kuamini kuwa mtu wa kawaida kama Oswald ana uwezo wa kutekeleza tukio lile ambalo lilipangwa kwa ustadi mkubwa sana.

Hii ndio inafanya watu waanze kuchanganua, kutafakari na kukuna vichwa kung'amua wahusika halisi wa tukio hili kwa kuzingatia umaridadi wa utekelezaji wake na 'motive'.

### MTUHUMIWA NAMBA 1: CIA

Kuna sababu nyingi sana na za msingi mno ambazo zinawatia 'hatiani' CIA juu ya uhusika wao katika kutekeleza mauaji ya Rais Kennedy.

Twende taratibu na hatua kwa hatua katika kuliangalia hili, tutaanzia mwanzo kabisa.

Kipindi ambacho Rais Kennedy anaingia madarakani Januari 20, 1961 aliikuta Marekani ikiwa vitani sehemu mbali mbali.

Kulikuwa na vita ya Vietnam ilikuwa inaendelea ambayo ilianza tangu mwaka 1955. Papo hapo pia Marekani walikuwa kwa siri kubwa wanaunga mkono vita ya wenyewe kwa wenyewe nchini Laos na wakiunga mkono familia ya kifalme ya nchini humo.

Pamoja na hayo yote kulikuwa na 'Tatizo' la Fidel Castro' ambalo lilikuwa linapaswa kutatuliwa na bila kusahau kwamba ni katika mwaka huo 1961 ndipo ambapo ukuta wa Berlin ulikuwa unajengwa.

Kwa hiyo kipindi ambacho Kennedy alikuwa anaingia madarakani alikuwa amerithi mitafaruku lukuki ya kimataifa kutoka kwa rais aliyepita Dwight Eisenhower ambayo ilikuwa inaikabili Marekani.

Migogoro yote hii ilikuwa ni mizito na ilikuwa imeiweka majaribuni Marekani kwa maana ya kwamba, katika kipindi hiki ndipo ambapo mvutano wa vita baridi kati ya Marekani na Uingereza ulikuwa umeanza kupamba moto hivyo Marekani ili kuendelea kubakiza imani za washirika wake juu ya uwezo wake wa kijeshi walikuwa wanapaswa kushinda.

Kuna masuala kadhaa ambayo JFK alikuwa anakubaliana nayo, moja kwa moja mwanzoni japokuwa yapo mengine ambayo alikuja kubadili msimamo huko mbeleni.

Mfano JFK alikuwa anaunga mkono na alikuwa na msimamo mkali wa kuhakikisha kuwa lazima Marekani ishinde vita ya Vietnam. Hii inadhihirishwa na kuongeza uwepo wa vikosi vya Marekani ni misaada kwa wapiganaji huko Vietnam mara 18 zaidi kushinda kipindi cha utawala wa rais Dwight Eisenhower. (japokuwa baadae JFK alianza kubadili msimamo).

Lakini kuna mgogoro kama wa Cuba dhidi ya Fidel Castro, kwenye suala kama hili JFK hakuwa na msimamo wa moja kwa moja bali alitegemea zaidi ushauri kutoka kwa vyombo vya usalama na ujasusi. Na ndipo hapa ambapo "mdudu akaingia kwenye kokwa la embe."

### HITIMISHO

Katika ripoti ya The Warren Commision, ile kamisheni iliyoundwa na Rais Lyndon B. Johnson kuna mahala inasema kwamba kuna mtu ambaye alijitambulisha kama "Clay Bertrand" alimpigia simu Dean Andrews Jr. ambaye alikuwa ni mwanasheria wa kujitegemea kwenye jimbo la New Orleans kumtaka apande ndege kwenda Dallas kumtetea Lee Harvey Oswald.

Lakini wajumbe wa Warren Commission wanadai kwamba walihangaika mno bila mafanikio na hawakujua huyu "Clay Bertrand" ni nani na wakafanya hitimisho kwamba hili halikuwa jina halisi bali ni 'alias' ambayo ilitumiwa tu na huyo mtu.

Ilipofika mwaka 1967 mwezi Machi, mwanasheria wa serikali wa New Orleans wa kipindi hicho aliyeitwa Jim Garrison alifanikiwa kung'amua huyu "Clay Bertrand" ni nani haswa.

Bw. Garrison aligundua kwamba kuna mfanyabiashara maarufu sana ambaye alikuwa anatumia "alias" hiyo kwenye jumuiya za watu wanaojihusisha na mambo ya ushoga.

Mfanyabiashara huyu maarufu sana miaka hiyo alikuwa anaitwa Clay Shaw.

Huyu alikuwa ni mwanzilishi wa shirika la 'International Trade Mart', ambapo shirika hili lilikuwa na lengo kuu la kuchochea biashara ya kimataifa na makao makuu yao yalikuwa ni New Orleans.

Vile vile nchini Italia Clay Shaw alikuwa ni mjumbe wa Bodi ya Kampuni ya CMC (Centro Mondiale Commerciale) ambayo ilikuwa ni 'subsidiary' ya kampuni mama inayoitwa Permindex (Permenent Industrial Expositions).

Sasa katika Ulimwengu wa Espionage na hata mambo ya uhalifu kuna kitu kinaitwa 'front organisations'. Hizi ni kampuni ambazo zinaanzishwa kwa siri na idara ya kijasusi kwa lengo la kutekeleza maslahi yake pasipo idara husika ya kijasusi kujulikana.

Na hii ndio inatoa sababu kwa baadhi ya wakubwa wa FBI siku za mwanzoni kabisa baada ya mauaji ya Kennedy kuanza kuwa na wasiwasi kwamba inawezekana kuna la zaidi.

Kuna nakala 'transcript' ya maongezi kati ya Mkurugenzi wa FBI Bw. Edgar Hoover na rais Lyndon Johnson yaliyofanyika Novemba 23, 1963 siku moja tu baada ya mauaji ya Kennedy. Nakala hii ilivuja mwaka 2006 kutoka kwenye files za FBI wenyewe;

### NUKUU YA NAKALA HII KAMA ILIVYO

Rais Johnson; "Have you established anymore about the (Oswald) visit to the Soviet Embassy in Mexico in September? (Kuna lolote umeling'amua juu ya (Oswald) kutembelea Ubalozi wa Urusi nchini Mexico?)

Hoover; "No, there is an angle that's very confusing for this reason. We have up there a man at the Soviet Embassy , using Oswald's name, do not correspond to this man's voice, nor to his appearance. In other words, it appears that there was a second person who was at the Soviet Embassy."

(Hapana, kuna upande wa suala hili unachanganya mno. Nahisi kuna mtu kule ubalozi wa Urusi anatumua jina la Oswald na hawarandani kwa sauti, wala kwa muonekano. Kwa maneno mengine, inaonekana kwamba tuna mtu mwingine tofauti wa pili anayeenda ubalozi wa Urusi na kujitambulisha kama Oswald).

Ni kwa nini CIA watumie nguvu nyingi hivi kumtengeneza mtu anayetumia jina la Oswald ambaye matendo yake yalisababisha kujenga image kwa Oswald halisi kwamba ni mwenye kufuata itikadi ya Ujamaa mkali na mwenye kuchukia umagharibi?

Ni kwa namna gani hasa CIA hatimaye walitekeleza tukio hili la mauaji? Nani ailifyatua risasi?

Kwenye miaka ya hivi karibuni baada ya uchunguzi wa kina na nyaraka nyingi kuvuja imethibitika kwamba kwenye miaka ya 1960s na 1970s, CMC na Permindex zilikuwa zinatumiwa kama 'front organisation' za CIA kwenye nchi ya Italia.

Kampuni hizi zilikuwa zinatumika kwa lengo kuu la kupitisha fedha kutoka CIA nchini Marekani na kwenda nchini Italia kugharamia mikakati ya kumwondoa madarakani Rais wa Italia kipindi hicho, Charles de Gaulle ambaye alikuwa na sera za kufungamana mno na Urusi na kupinga vikali siasa za kimagharibi.

Katika Bodi hiyo hiyo ya Kampuni ya Permindex (na CMC) pia kulikuwa na mjumbe mwingine wa Bodi aliyeitwa Loius Bloomfield.

Huyu alikuwa ni msomi wa hali ya juu na mfanyabiashara maarufu kutoka Canada ambaye kipindi cha uhai wake alionekana na wengi kama kiongozi wa jamii ya Wayahudi nchini Canada.

Lakini ikumbukwe kwamba, Louis Bloomfield wakati wa vita kuu ya pili miaka ya 1940s aliitumikia idara ya kijasusi ya kimarekani iliyoitwa 'Office of Strategic Services'.

Idara hii ndio baadaye (baada ya vita kuu ya pili) ilibadilishwa jina na kuitwa 'Central Intelligence Agency '- CIA ambayo tunayo mpaka sasa.

Kwa maneno mengine mjumbe huyu wa Bodi ya Permindex alikuwa ni jasusi nguli na hata kampuni yao hiyo (Permindex na CMC) kama ambavyo nimeeleza zilikuwa ni 'front organisation' za CIA.

Kwa hiyo basi kitendo cha mfanyabiashara maarufu Clay Shaw ambaye mwanasheria wa serikali Garrison aling'amua ndiye huwa anatumia a.k.a ya "Clay Bertrand", kitendo chake cha kuwa pia mjumbe wa Bodi ya CMC na Permindex inadhihirisha mafungamano yake na CIA na shughuli za kijasusi.

Hivyo basi, bila kuogopa mafungamano ya Clay Shaw na CIA, Mwanasheria Mkuu wa New Orleans, Jim Garrison alimkamata Clay Shaw siku ya Machi 1, 1967 na kumfungulia mashtaka ya kupanga njama ya kumuua Rais Kennedy.

Katika hati yake ya mashataka, Garrison alieleza pia kinaga ubaga kuwa CIA wamehusika pia kwenye tukio hilo.

Wakati wa kusikilizwa kwa kesi hiyo,Garrison alieleza mahakama sio tu kwamba Clay Shaw ndiye mwenye kutumia alias ya "Clay Bertrand" ambaye alikuwa anatafutwa miaka yote, bali pia alimleta shahidi wake aliyeitwa Perry Russo ambaye alikuwa ni mfanyabiashara mkubwa wa masuala ya Bima.

Shahidi huyo alieleza Mahakama kuwa alihudhuria tafrija nyumbani kwa bwana mmoja anaitwa David Ferrie ambaye anajulikana kuwa moja ya wapinzani wakubwa wa utawala wa Fidel Castro.

Shahidi akaeleza kuwa akiwa kwenye tafrija hiyo kwa bahati mbaya aliwasikia Clay Shaw, David Ferrie na watu wengine wachache ambao hakuwatambua walikuwa wamekaa chemba wakipeana maelekezo fulani kuhusu mpango huo.

Kesi hii iliunguruma kwa muda wa miaka miwili mfululizo. Lakini ajabu ni kwamba siku ya tarehe 1, Machi 1969, Baraza la Wazee wa Mahakama (Jury) walikaa kwa muda wa chini ya nusu saa na kutoa uamuzi wa pamoja wa kumuachia Clay Shaw kuwa huru dhidi ya mashtaka yote hayo.

Hii ilikuwa habari njema kwa CIA lakini umma ulijawa na hasira na hasira hizi walizielekeza moja kwa moja kwa Clay Shaw.

Mwaka 1974 siku ya tarehe 15 Agosti, Clay Shaw alifariki kwa "Kansa ya Mapafu".

Kama ambavyo Jack Ruby (yule aliyempiga risasi Oswald) naye alifariki kwa "Kansa ya Mapafu" akiwa gerezani.

Na msururu mrefu wa kila ambaye alionekana kujua uhalisia wa mauaji ya Kennedy alifariki muda mchache tu katika mazingira ambayo yanazua maswali mengi.

Si vema kutoa hitimisho la moja kwa moja katika makala kama hii, ni vizuri msomaji asome, aone 'facts' na kisha yeye mwenyewe binafsi afanye hitimisho lake.

Lakini katika tukio hili la mauaji ya Rais JF Kennedy, CIA hawawezi kuruka ukweli kwamba mikono yao ina damu yake.

**MWISHO**

# Kiongozi wa upinzani mahakamani akituhumiwa kupanga kumuua Rais



**LILONGWE, Malawi**

KIONGOZI wa chama cha upinzani nchini Malawi, Patricia Kaliati, ameshtakiwa kwa kupanga njama za kumuua Rais wa nchi hiyo, Lazarus Chakwera.

Patricia, Katibu Mkuu wa chama cha UTM, alikamatwa wiki iliyopita kwa tuhuma za kula njama na wengine kutenda kosa kubwa.

Alipofikishwa juzi Jumatatu katika Mahakama katika Mji Mkuu wa Malawi, Lilongwe, mwanamama huyo mwenye umri wa miaka 57, hakuzungumza.

Lakini wakili wake alidai kuwa mwanasiasa huyo alisisitiza kuwa hana hatia, ripoti ya vyombo vya habari vya ndani zinaeleza.

Maelezo machache ya madai ya njama hizo, yametolewa na viongozi mbalimbali wa upinzani wanadai kuwa mashitaka dhidi ya Kaliati yamechochewa kisiasa.

Wafuasi wa UTM walikusanyika nje ya Mahakama na kuimba nyimbo za kuipinga serikali kabla ya kusikilizwa kwa kesi, kwa mujibu wa Shirika la Habari la AFP.

Ndani ya mahakama hiyo, Mahakama iliambiwa kwamba Partricia alikuwa na washiriki wawili, waliosemekana kuwa walikimbia.

Hatimaye hakimu aliamua kwamba Partricia anaweza kuachiliwa kwa dhamana huku uchunguzi ukiendelea.

Mwendesha Mashitaka wa Serikali alikuwa ameomba azuiliwe kwa wiki nyingine.

Polisi nchini Malawi walisema wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria na kwamba haki za Partricia zitaheshimiwa.

BBC.

> **Mwendesha Mashitaka wa Serikali alikuwa ameomba azuiliwe kwa wiki nyingine.**

# Mpinzani wa Ujerumani atiwa kitanzi kwa kuongoza ugaidi

**TEHRAN, Iran**

IRAN imemnyonga mpinzani wa Ujerumani na Iran Jamshid Sharmahd, baada ya kukutwa na hatia ya "kuongoza operesheni za kigaidi", vyombo vya habari vya serikali vinaripoti.

Sharmahd alihukumiwa kifo mwaka jana baada ya kushutumiwa kwa kuongoza kundi la wafuasi wa kifalme lenye makao yake makuu nchini Marekani.

Alikuwa amekanusha mashtaka, huku familia yake ikisema kuwa yeye ni msemaji tu. Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani alisema Berlin imeonya mara kwa mara Tehran kuwa kunyongwa kwa raia wa Ujerumani "kutakuwa na madhara makubwa".

"Kuuawa kwa Jamshid Sharmahd kunaonesha ni aina gani ya sheria za utawala zisizo za kibinadamu (nchini Iran)," Annalena Baerbock alichapisha kwenye X.

Mashirika ya haki za binadamu yamelaani kunyongwa kwa Sharmahd, ambaye aliishi Marekani.

"Mchakato mzima, ikiwa ni pamoja na kukamatwa kwake, kuhukumiwa, na kunyongwa, ni ukiukaji mkubwa wa sheria za kimataifa," alisema Mahmood Amiry-Moghaddam, mkurugenzi wa kundi la Haki za Kibinadamu la Iran lenye makao yake makuu nchini Norway.

BBC.



# Jeshi la Mali laua magaidi 40

**BAMAKO, Mali**

JESHI la Mali limesema limewaua takriban magaidi 40 na kuharibu moja ya ngome zao katika operesheni mbili zilizofanyika nchini humo.

Operesheni hizo zilizofanyika Alhamisi na Ijumaa wiki iliyopita, ziliharibu ngome katika mji wa Ounguel.

Operesheni ya Alhamisi katika mji huo iliharibu ngome moja na kuwaua takriban magaidi 30 huku risasi, silaha na pikipiki 24, zikikamatwa, wakati operesheni iliyofanyika Ijumaa ilifanikisha kuuawa kwa wanamgambo 10 pamoja na kukamatwa bidhaa kadhaa ikiwemo magari na pikipiki.

Mali ambayo inakabiliana na migogoro ya kisiasa, usalama na uchumi, imekuwa ikiandamwa na makundi ya kigaidi ya Al-Qaeda na lile linalojiita dola la Kiislamu tangu mwaka 2012.

DW.

# UNRWA lapigwa `stop' kufanya kazi Israel

**YERUSALEM, Israel**

BUNGE la Israel limepiga kura kupitisha sheria ya kupiga marufuku Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Palestina (Unrwa) kufanya kazi ndani ya Israel na Yerusalem Mashariki inayokaliwa na Israel, ndani ya miezi mitatu.

Mawasiliano kati ya wafanyakazi wa Unrwa na maafisa wa Israel, pia yatapigwa marufuku na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa uwezo wa shirika hilo kufanya kazi huko Gaza na Ukingo wa Magharibi unaokaliwa na Israel.

Ushirikiano na Jeshi la Israel ambalo linadhibiti vivuko vyote vya Gaza ni muhimu kwa Unrwa kuhamishia misaada katika eneo lenye vita. Ni shirika kuu la Umoja wa Mataifa linalofanya kazi huko.

Wafanyakazi wa Unrwa hawatakuwa tena na kinga ya kisheria ndani ya Israel, na makao makuu ya shirika hilo huko Jerusalem Mashariki yatafungwa.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, António Guterres, alisema kutekeleza sheria hizo kutakuwa na madhara kwa utatuzi wa mzozo wa Israel na Palestina na kwa amani na usalama katika eneo kwa ujumla, huku Mkuu wa Unrwa Philippe Lazzarini akisema itazidisha mateso ya Wapalestina.

Nchi kadhaa, zikiwemo Marekani, Uingereza na Ujerumani, zimeelezea wasiwasi wake mkubwa kuhusu hatua hiyo. Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza David Lammy aliiita makosa kabisa, wakati Waziri Mkuu Sir Keir Starmer alisema sheria zinahatarisha kufanya kazi muhimu ya Unrwa kwa Wapalestina isiwezekane, na kuhatarisha mwitikio mzima wa kibinadamu wa kimataifa huko Gaza".

BBC.




# Botswana kufanya uchaguzi leo

**GABORONE, Botswana**




BOTSWANA leo Jumatano inafanya uchaguzi wake mkuu ambapo Rais Mokgweetsi Masisi, anashindana na wagombea wengine watatu, akitafuta muhula wa pili kwenye taifa hilo lenye utajiri mkubwa wa almasi.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Reuters, uchaguzi huo huenda ukawa na ushindani mkali kulingana na wachambuzi ingawa upinzani uliogawanyika, unatoa nafasi kubwa kwa chama cha Masisi cha Botswana Democratic Party (BDP), ambacho kimetawala taifa hilo la watu milioni 2.3 tangu kujipatia uhuru wake kutoka kwa Uingereza mwaka 1966.

Botswana imekuwa na ustawi kwa muda mrefu, zaidi kutokana na utajiri wa almasi pamoja na idadi ndogo ya watu ambao hupewa huduma za bure za elimu na afya.

Hata hivyo, kushuka kwa bei ya almasi kwenye soko la kimataifa katika miaka ya karibuni, kumesababisha kushuka kwa mapato ya ndani, wakati taifa likijitahidi kuwekeza kwenye sekta nyingine.

Wapinzani wanasema kuwa chama cha BDP, kimebaki madarakani kwa muda mrefu zaidi na kwa hivyo kulaumiwa kuvuruga uchumi pamoja na ufisadi, madai ambayo kimekanusha. Wakati wa mdahalo uliofanyika wiki iliopita, Masisi alisema kuwa ni kweli almasi hazinunuli tangu Aprili, mwaka huu na kwamba uchumi umeshuka, lakini mfumo wa kiuchumi ungali dhabiti.

VOA.

# Miaka 29 bila Jabali la Muziki Marijani

## ● Anaendelea kukumbukwa kwa tungo zake zisizochuja

**Na Hamid Yassin**

IMETIMIA miaka 29 na ushei sasa tangu Jabari la Muziki nchini, Marijani Rajabu afariki dunia Machi 23 mwaka 1995.

Historia ya gwiji huyu ilianzia siku alipozaliwa tarehe 3 Machi mwaka 1955, katika eneo la Kariakoo. Mama yake alikuwa mama wa nyumbani wakati baba yake alikuwa anafanya shughuli za uchapishaji.

Maisha yake ya utoto yalikuwa ya kawaida ila alikuwa akipenda sana uimbaji wa Tabu Ley na mwimbaji mmoja wa Guinea Sorry Kandia. Alisoma shule ya msingi ikiambatana na elimu ya madrasa. Mwaka 1970 Akiwa bado shuleni, utaona umri wake ulikuwa miaka 15 tu, alijiunga na STC Jazz, ikiwa chini ya mpiga gitaa maarufu wakati huo, Raphael Sabuni, kabla ya hapo bendi hii ilikuwa ikijulikana kama The Jets.

Katika bendi hii Marijani aliweza kutoka nje ya Tanzania kwa mara ya kwanza ambapo alikwenda Nairobi na kurekodi nyimbo zilizotoka katika label ya Phillips.

Hili jambo la mwanafunzi kusafiri na bendi likaleta shida na kwa vile (STC) ilikuwa mali ya umma akaachishwa kazi na mwaka1972 alijiunga na The Trippers ya David Mussa ambayo kwa wakati huo ilikuwa inapiga zaidi nyimbo za hoteli na za kukopi na mwimbaji wao kiongozi wakati huo alikuwa Ali Rajabu.



Marehemu Marijani Rajabu (kushoto)

**SAFARI TRIPPERS**

Hapa ndipo ubora wake ulifunguka haswa na kuweza kuinyanyua Trippers, ambayo sasa ilibadili jina na kuwa Safari Trippers kutokana na msimamo wa serikali wakati huo wa kutaka majina ya nyumbani yatumike badala ya yale ya kigeni na kuwa moja ya bendi maarufu za wakati huo.

Waliweza kutoa vibao vilivyopendwa mfululizo na kuweza kuzunguka nchi nzima. Vibao kama 'Rosa Nenda Shule', 'Georgina', 'Mkuki Moyoni', 'Sikitiko', 'Mateso', 'Mtoto wa kambo', 'Mayasa', 'Sauti yako nyororo', 'Masudi', 'Kombora', 'Pendo si kulazimisha', 'Mkuki moyoni' wa David Mussa na nyinginezo ambazo viliweza kuuza zaidi ya nakala 10,000 za santuri na hivyo kuwezesha bendi kuwa na vyombo vyake vizuri.

Bendi wakati huo ikiwa na wanahisa wanne, ambao kwa bahati mbaya wakati bendi ndio iko juu, wakakosa kuelewana na ukawa ndio mwisho wa bendi hiyo.

Marijani alishiriki kutunga, kuimba nyimbo karibu zote za Trippers sanjari na kupiga gitaa kwa baadhi ya nyimbo. Mfano wimbo 'Olila' ambao alipiga rhythm na kuimba.

**DAR ES SALAAM INTERNATIONAL**

Mwaka 1976, Marijani na baadhi ya wanamuziki wa Trippers waliamua kuihama bendi na kwenda kuasisi Dar es salaam International chini ya umiliki wa Mzee Zakaria Ndabemeye.

Baadhi ya wanamuziki hao ni pamoja na Abel Baltazar kutoka Msondo, Kassimu Mponda kutoka Trippers, Abdallah Gama, Joseph Mulenga, Haruna Lwali na George Kessy Omojo waliokuwa wanapiga muziki Magot, Said Mohamed kutoka Polisi Jazz, Cosmas Chidumule kutoka Urafiki, Belesa Kakere kutoka Biashara Jazz, Joseph Bernard kutoka Trippers, Ali Rajabu kutoka Trippers, na King Michael Enock kutoka Dar es Salaam Jazz.

Akiwa Dar International alishiriki kutunga nyimbo mbili, 'Betty' na 'Sikitiko'. Hata hivyo kama Waswahili wanavyosema mafahari wawili hawakai zizi moja ndivyo ilivyotokea kati yake na Abel Balthazal kiasi cha hatimaye Marijani kufukuzwa ndani ya bendi kutokana na ubishi kuhusu wimbo aliotunga Marijani.

Kuna maelezo kuwa, wimbo huo ulionekana unafanana na wimbo fulani toka Congo DR na hivyo Marijani akatakiwa aubadilishe na ndipo ugomvi ukaanza.



Marehemu Marijani Rajabu ( wa pili kutoka kulia)

Hata hivyo mwishoni mwa mwaka 1978, Marijani alirejeshwa tena kundini kutokana na rundo la wanamuziki wa Dar International kuihama bendi kwa kishindo kikubwa na kwenda kuifungua bendi mpya kabisa ya Orchestra Mlimani Park.

Aliporejeshwa Marijani alikuja na wanamuziki wengi wapya wakati huo kama akina Christopher Kasongo, Mohamed Tungwa, Mafumu Bilal, Hamis Milambo, Athuman Momba, Mzee Alex Kanyimbo na wengine na kuja na mtindo wa Super Bomboka.

Katika kudhihirisha hasira zake kwa Abel, Marijani alimtungia Abel wimbo wa kumnanga ukiitwa 'Kidudu Mtu' ambao hata hivyo RTD waliukataa kuurekodi, jambo lililokuwa kawaida enzi hizo kwa redio kukataa wimbo.

Sifa nyingine ambayo Marijani alikuwa nayo ni kuibua wanamuziki chipukizi kama alivyofanya mwaka 1983 alipomuibua kutoka Tanga kijana Mkuu Waziri Kungugu Kitanda Milima Al maarufu Fresh Jumbe ambaye kwa hakika kabisa Marijani hakujutia kumchukua kijana huyo.

Alimwamini kupita maelezo kiasi kwamba wakati mwingine alikuwa akimuachia bendi aongoze na yeye anapumzika nyumbani. Mbali na Fresh, wanamuziki wengine ni kama vile Tino Masinge, Mohamed Mwinyikondo, Juma Choka na wengine kibao.

Baada ya kurekodi 'Zuena' na 'Mwanameka' na nyimbo nyingine katika albamu hiyo alichoambulia ni malipo ya nauli toka RTD ya sh. 2500/- tu. Kilichosikitisha zaidi ni kuwa nyimbo zao tisa ziliuzwa kwa kampuni ya Polygram bila ridhaa yao.

Hata hivyo, safari ya Dar International ilikoma mwaka 1987 kutokana na sababu za kawaida za kufa kwa bendi lakini kubwa ni uchakavu wa vyombo.

Marijani aliendelea kufanya muziki na kwa kipindi kifupi amewahi kucheza na Kurugenzi ya Arusha na Mwenge Jazz ambayo alirekodi nayo wimbo mmoja wa 'Ukimwi' na hata kupitia bendi ya Watafiti.

Mwaka huo huo wa 1987 Marijani na Muhidin Maalim Gurumo waliliongoza kundi la wanamuziki zaidi ya 50 kutunga nyimbo maalum hasa kwa maadhimisho ya miaka 10 ya CCM na 20 ya Azimio la Arusha. Kundi hilo lilijulikana kwa jina la Tanzania All Stars. Aidha mwaka 1994 aliwahi kurekodi 'zing zong' na marehemu Eddy Sheggy.

Bendi yake ya mwisho ilikuwa ni Africulture ama Mahepe Ngoma ya Wajanja, iliyokuwa mali ya Rogers Malila, alikokuwa na wanamuziki kadhaa kama akina Hassan Kunyata, Mgosi na wengine.

Bado Marijani ataendelea kukumbukwa na wapenda muziki kote nchini na hata Afrika kwa ujumla kwa nyimbo zake zenye mafundisho na tamu huku akienzi utamaduni na ngoma za kwao Kigoma.

**Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.**

# Ngumi; Mchezo unaorudishwa nyuma na wadau wake




**Na Hamid Yassin**

MASUMBWI au kwa majina mengine ndondi au ngumi na kwa majina ya mitaani ndonga, mawe, ni mchezo unapoendwa sana na watu wengi sambamba na kuogopwa sana duniani.

Mchezo wa ngumi uko hatarini kupoteza msisimko wake hususani huku kwa zile za kulipwa kutokana na mitafaruku ya mara kwa mara miongoni mwa wadau wake.

Huko miaka ya nyuma , mchezo wa ngumi ulichezwa kama burudani, kuwakilisha nchi na kujenga ushupavu wa mchezaji, lakini baada ya kuingia ngumi za kulipwa umegeuka kuwa wa kupanda na kushuka kinyume na mategemeo ya wengi..



## MFUMO FEDHA NA TAA INAYOZIZIMA

Kama nilivyoelezea hapo mwanzo, ngumi zilichezwa kwa ushindani mkubwa kuwakilisha nchi katika mashindano ya ridhaa, lakini ulipoingia kwenye hizi za kulipwa wadau wake wamekuwa wakiupeleka arijojo kila pale unapotoa mwanga mzuri wa matumaini.

Mabondia wengi wa miaka ya sasa toka hapa nchini na Afrika Mashariki na Kati wanashiriki tu kwenye mapambano kwa lengo la kupata fedha za kujikimu, lakini si kujikwamua kimaisha kama ilivyo kwa wenzao kwenye nchi zilizoendelea hata na kule bara la Asia,

Wengi wa mabondia hawa hutoroshwa kwenye nchi zao kimyakimya na mameneja feki wenye lengo la kuwatumia kujipatia fedha. Mabondia wengi wa zamani wamegeuka kuwa mawakala feki na mameneja wa hawa mabondia wa sasa kwa lengo la kuwatumia zaidi kwa manufaa yao.

Mabondia wengi toka nchi za Afrika Mashariki wanatapeliwa fedha nyingi na mameneja ama mapromota hawa feki baada ya kucheza mapambano katika nchi za Ulaya, Asia na hata Afrika.

"Fedha" na sio kitu kingine chochote kinachokuwa msukumo wa wanamasumbwi wengi wa Kitanzania kucheza ngumi. Kuna mapromota wengi wa nje ambao hutaka mabondia dhaifu ama wale walio tayari kusafirishwa nje ya nchi kwa masharti kwamba huko lazima wakubali kwenda kushindwa na sio kushindana!

Hii ni kwa sababu wanataka kuwatengenezea rekodi nzuri mabondia wao wa huko ughaibuni. Yapo madai toka kwa mameneja hawa matapeli ambapo wanaomba bondia wa Kitanzania aandaliwe pambano feki hapa nyumbani ili rekodi yake ikubalike na shirikisho la nchi yake na hatimaye kumsaidia kumpandisha viwango bondia wake.

Mchezo wa ngumi umepoteza mwelekeo sio tu hapa Tanzania bali dunia nzima. Mameneja / mapromota wengi huwatengeneza mabingwa nje ya ulingo badala ya kuwaacha mabondia wao wawe mabingwa wa kweli.

Kwa kawaida bondia bingwa anatakiwa awe amewashinda mabondia karibu wote walio kwenye uzito / kiwango chake ndipo ajulikane kama bingwa.

Lakini mabingwa wa sasa wanatengenezwa toka pambano la kwanza kwa kupambanishwa na mabondia hafifu ili awashinde na kutengeneza rekodi nzuri. Wapo mabingwa wengi wa dunia waliotengenezwa kwa njia hii badala ya kuwa mabingwa kwelikweli. Hii yote ni kwa ajili ya fedha.

Na mabondia wetu wengi wa ukanda wetu wa Afrika ndiyo wahanga wakugeuzwa 'panching bag' na wale mapromota feki wanaotaka kuwanyanyua mabondia wao mbeleko ya chuma.

Bingwa yeyote anapotakiwa atetee ubingwa wake hupewa donge nono. Kwa bingwa anayetambuliwa na mashirikisho kama WBA, IBF, WBO na WBC donge la fedha analopewa ni kubwa zaidi.

Mameneja wengi hutumia fedha kuwaingiza mabondia wao kwenye viwango vya mashirikisho haya ili kuwaweka katika orodha ya kuelekea kwenye ubingwa.

Mara tu bondia anapokuwa bingwa hujihakikishia ulaji na meneja / promota wake anamchagulia wapinzani wasioweza kumnyang'anya ubingwa huo ili aendelee kutulia nao.

Bingwa huyu anaweza kukaa na ubingwa kwa muda mrefu sana. Mfumo wa sasa wa ngumi unalenga kuwanufaisha wale walio na bondia kama mameneja, promota, wakala, waandaaji wa mapambano 'matchmakers' na mabondia wengine. Mfumo fedha unadidimiza mchezo wa ngumi.

Kuna makubaliano na ushirikiano mkubwa sana wa siri kati ya meneja, promota na baadhi ya mashirikisho husika ili bondia aweze kuwa bingwa na atetee ubingwa wake kwa muda mrefu.

Hali hii japokuwa inadhibitiwa kwa kiasi kikubwa miaka ya karibuni bado imechangia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa mchezo huu kidunia.

Miaka ya karibuni makundi (rackets) kama hizi zilizogundulika na kuwekwa wazi kwenye Shirikisho la Ngumi la Kimataifa (IBF). Rais wa zamani wa IBF Bob Lee Sr. pamoja na maofisa wengine walitiwa hatiani kwa kosa la kuwatengenezea mabondia ulaji kama huu.

Walisemekana kuwa walidai kiasi cha dola kama 300,000 ili bondia apandishwe kiwango na achezee ubingwa. Bob Lee Sr. na wenzake walikumbwa na kashfa hii na kuondolewa IBF.

Japokuwa mashirikisho mengi ya ngumi bado yanaendelea na uozo huu ni juhudi ndogo sana zinazofanywa kuwabana. Ilikuwa rahisi kwa IBF kubanwa kwa kuwa sheria za nchi ya Marekani zilitumika.

Mengi ya mashirikisho ya ngumi yapo nje ya sheria za Marekani na sio rahisi kuwadhibiti. Badala yake juhudi nyingi zinafanywa na mabondia wachache kwa kufungua kesi za madai mahakamani ili kuweza kupata haki zao.

Mameneja / mapromota nao hawako nyuma kwenye kashfa mbalimbali za ngumi zinazohusu utumiaji wa fedha za mabondia na hata kuwatibulia kuwa mabingwa.

Ziko kesi nyingi kwenye mahakama huko Ulaya na Marekani ambazo mabondia wanawadai mameneja / mapromota mamilioni ya fedha. Mara nyingi kesi hizi humalizwa nje ya mahakama kwa makubaliano.

Sheria kali zinazoendesha mchezo huu zinatakiwa zifuatwe na udhibiti uwe wa hali ya juu. Sio rahisi kupata mafanikio katika mchezo huu bila sheria hizi kufuatwa na kila mdau.

"Niletee bondia asiye mkali ili asimpe shida bondia wangu. Mtengenezee pambano la kumpandisha rekodi yake. Mtengenezee leseni mpya inayoonyesha rekodi nzuri," haya ni mazungumzo ya kawaida kwenye ngumi za kulipwa duniani.

Haya ni baadhi tu ya maelekezo yanayotoka kwa mameneja wa nje wanapotafuta bondia wa Kitanzania kwenda kucheza huko nje. Kuna kundi kubwa la mameneja hawa uchwara ambao wanashirikiana na mawakala wa kila aina hapa Afrika.

Wengi wa mawakala hawa kama nilivyokwisha eleza hapo mwanzo ni mabondia wa zamani na wafanyabiashara wanaotumia nafasi ya kumpeleka bondia nje ili wakanyooshe mambo yao.

Inapotokea safari ya nje kwa bondia wafanyabiashara hawa hawawezi hata kuwa-sekondi (kuwahudumia) mabondia kwenye kona zao na badala yake wanawaachia wageni wa nchi wanayochezea kufanya kazi hiyo.

Ni wazi kwamba bondia anapohudumiwa na mgeni tena anayetaka ashindwe ana nafasi ndogo sana ya kufanya vizuri. Wengi wa wahudumu hawa hawaelewani hata lugha na bondia mwenyewe!

Safari nyingi za mabondia wetu siku hizi wanatakiwa wasafiri wenyewe ili eti wawakute wahudumu nchi wanayokwenda. Kwa kawaida kila bondia wanatakiwa asafiri na meneja na kocha wake.

**Kwa ushauri na maoni; 0768 888 787 ama 0784 122 020.**

# Ademola; Mwafrika pekee aliyewania tuzo ya Ballon d'Or

**Zurich, Switzerland**




ADEMOLA Lookman, winga huyo toka Nigeria alichukua vichwa vya habari kote Ulaya na Afrika kuanzia uchezaji wake akiwa na Super Eagles (Nigeria) wakati wa Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023, hadi kuisaidia Atalanta kushinda taji lao la kwanza la UEFA, nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 anaendelea kuinuka.

Maendeleo ya Lookman yalimfanya aorodheshwe kama mmoja wa wachezaji 30 walioteuliwa kuwania tuzo ya Ballon d'Or mwaka huu, mshindi wa tuzo hiyo ya mwanasoka bora zaidi duniani ni Mhispania, Rodrigo Hernandeg wa Manchester City aliyetangazwa jijini Paris juzi Jumatatu.

Kuwa Mwafrika pekee kwenye orodha hiyo kumeongeza uzito katika mafanikio yake.

"Ni jambo kubwa kuwa kwenye orodha na jambo kubwa zaidi kuwa Mwafrika pekee," anasema.

Moja ya wakati wa furaha kwa Lookman ilikuwa ni katika fainali ya UEFA, alifunga mabao matatu na Atalanta ikapata ushindi dhidi ya timu ya Bayer Leverkusen.

Uchezaji wake kwenye uwanja wa Aviva mjini Dublin ulionyesha ustadi wake, na akawa mchezaji wa kwanza kufunga magoli matatu katika fainali ya UEFA tangu Jupp Heynckes alipoifungia Borussia Monchengladbach katika Kombe la Uefa la 1975.

"Usiku huo ulikuwa wa kipekee," anakumbuka Lookman.

**ALIKOTOKEA**

Amekuliwa Kusini mwa London na kuanza kucheza mpira katika timu ya vijana ya Charlton Athletic.

Lookman alijiunga na Everton kwa mkataba wa pauni milioni 11 alipokuwa na umri wa miaka 19, na kisha akahamia katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani.

Alirudi kwenye Ligi ya Kuu ya Uingereza kwa mkopo, akianza kucheza Fulham na kisha Leicester City, lakini fowadi huyo aliimarika zaidi tangu alipohamia Atalanta mwezi Agosti 2022.

Kuhamia nchi mpya, kujifunza lugha mpya na kuzoea utamaduni tofauti wa soka kunaweza kuwa jambo la kuogofya, lakini Lookman anastawi huko kaskazini mwa Italia.

Miaka yake miwili akiwa Bergamo imekuwa ya mabadiliko na anaamini mtindo wa uchezaji wa klabu hiyo chini ya kocha Gian Piero Gasperini umempa fursa ya kuonyesha ubunifu wake uwanjani.

Kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu kumempa Lookman fursa nyingine ya kuonyesha ujuzi wake dhidi ya timu bora zaidi duniani

**MNIGERIA MOYONI**

Licha ya mafanikio yake ya mapema akiwa na timu za vijana za England, ikiwa ni pamoja na kushinda Kombe la Dunia la Chini ya miaka 20 mwaka 2017, lakini alimuamua kuiwakilisha Nigeria katika ngazi ya juu ya soka.

"Siku zote mimi ni Mnigeria, niliyezaliwa na kukulia nchini Uingereza," anasema.

"Siku zote niko karibu na watu wangu, na utamaduni wangu. Nimekuwa nikienda na kurudi Nigeria tangu nikiwa mtoto."

Uamuzi wa kubadili utiifu na kuichezea Nigeria Mwaka 2022 ulirahisishwa na uhusiano wake wa asili na urithi kwa nchi hiyo.

"Ni heshima kuwa na nembo ya Nigeria kifuani mwangu na kuweza kuivaa kwa fahari."

Uchezaji wake akiwa na Super Eagles umemfanya kupendwa na mashabiki na alikuwa mchezaji muhimu katika timu hiyo kuelekea mechi za AFCON 2023.

Mabao matatu ya Lookman nchini Ivory Coast yalimfanya atajwe kwa sifa katika michuano hiyo, lakini Nigeria ilichapwa 2-1 kwenye fainali na wenyeji.

Wakati mafanikio ya Lookman katika klabu yakiongezeka, Nigeria imekumbwa na changamoto mwaka huu.

Juhudi za timu kuwania kufuzu Kombe la Dunia la 2026 la FIFA zimekosa utulivu, kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya wakufunzi.

Licha ya changamoto hizo, Lookman bado ana matumaini kuhusu mustakabali wa timu hiyo, wakati mechi za kufuzu AFCON 2025 zikikamilika mwezi ujao.

"Kila mtu anajua tuna kikosi kilichojaa vipaji. Na tunapocheza pamoja, tutaonyesha hilo zaidi. Sote tunafanya kazi kwa bidii kuelekea lengo moja."

Licha ya mafanikio yake mwaka 2024, Lookman hayuko tayari kupumzika; "Ninalenga kuendelea kupigania mambo ninayotaka."



## Kona ya Urembo



# Muonekano nadhifu wa vazi la Mama Samia







**Na Hidaya Machupa**

VAZI la Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, limekuwa na mvuto mkubwa na umaarufu ndani na nje ya Tanzania. Mara nyingi Rais Samia huvaa mavazi ya Kiafrika yaliyojaa rangi mbalimbali, lakini akijitofautisha na mtindo wa kipekee wenye heshima na unaoendana na nafasi yake ya uongozi.

Mojawapo ya mavazi maarufu anayovaa ni kanga, batiki, au vitenge vilivyoshonwa kwa mtindo wa kisasa lakini vikiheshimu mila za Kiafrika. Kanga ni vazi la kitamaduni linalopendwa sana Afrika Mashariki, na mara nyingi limewekwa maandiko yenye ujumbe wa hekima au nasaha.

Aidha, Rais Dk. Samia huvalia hijabu nyepesi yenye kufunika kichwa, kitu ambacho kinatoa mfano wa uvaaji wa heshima unaokubalika kwa jamii mbalimbali.

Huu ni mtindo ambao umejikita katika maadili ya uongozi na kuthamini utamaduni wa Mtanzania na wa Kiswahili. Vazi lake linatoa picha ya kiongozi anayeishi kwa kuzingatia asili, huku akihimiza utambulisho na fahari ya Kiafrika.

Rais Dk. Samia ameweza kuchanganya urembo wa asili na mitindo ya kisasa kwa ustadi, akijenga taswira ya kiongozi mwenye heshima na uzalendo.

Mara nyingi hupendelea mitindo ya rangi tulivu kama vile bluu, kijivu, na kijani iliyopambwa na vitambaa vya kitenge au kanga, ambavyo vina rangi angavu zinazowakilisha urithi wa Kiafrika.

Hii inaonesha si tu mapenzi yake kwa utamaduni wa Afrika Mashariki, bali pia hali ya umakini na heshima kwa nafasi yake kama kiongozi wa kitaifa.

### MAPAMBO

Kwa upande wa mapambo, Rais Dk. Samia hupendelea mtindo wa kawaida, usio mzito. Huweka mapambo ya kawaida, kama hereni ndogo na bangili zisizovutia macho kwa sana, akihakikisha kuwa mwonekano wake unadumisha unyenyekevu na si wa kupindukia.

Makeup yake ni nyepesi na hutumika kwa umakini ili kuongeza mvuto wa asili huku akidumisha umakini wa kitaaluma.

Urembo na mitindo ya Rais Dk. Samia ni kielelezo cha uongozi wa kisasa unaozingatia urithi wa Kiafrika, ukionesha kuwa kiongozi anaweza kuwa na mtindo mzuri bila kupoteza heshima na weledi. Huu ni mfano bora kwa wanawake wengi barani Afrika na kwingineko.

### WANAYOPENDEKEZA WADAU

Baadhi yao wamependekeza mambo kadhaa ambayo yanaweza kuboresha zaidi mwonekano wake bila kupoteza uzito na utulivu wa mavazi yake.

### MATUMIZI YA RANGI ZA KUINUA MVUTO

Wataalamu wanasema kuwa Rais Dk. Samia anaweza kuendelea kutumia rangi zilizotulia, lakini wakati mwingine kuongeza rangi nyepesi kama dhahabu au nyekundu kwa mapambo madogo kwenye mavazi ili kutoa mvuto na nguvu kwenye mwonekano wake wa jumla.

### KUBADILISHA VITAMBAA NA MIFUMO YA KIPEKEE

Imependekezwa kwamba, anapovaa kitenge au kanga, anaweza kuchagua vitambaa vyenye mifumo ya kipekee inayochora ramani au ishara za kiutamaduni, ili kusisitiza zaidi utambulisho wa Kiafrika. Vitambaa hivi vinaweza kufanywa maalum kwa ajili ya ofisi au matukio rasmi.

### MITINDO YA VAZI LENYE UMBO BORA

Kwa kuwa ni kiongozi wa juu, wataalamu wanashauri mavazi yanayokaa vizuri kwenye mwili bila kuwa mazito sana. Mavazi yenye mikato midogo midogo inaweza kusaidia kuongeza mwonekano wa kitaalamu na wa kisasa.

Hii inajumuisha makoti na suti zilizoshonwa kwa umaridadi bila kupoteza uhalisia wa mavazi ya Kiafrika.

### MAPAMBO YA ASILI NA VIPULI VYA KISASA

Ijapokuwa Rais Samia hupendelea mapambo machache, wataalamu wanashauri kuchanganya vipuli na bangili za asili au vya kisasa, kama za fedha au shaba nyepesi, ambazo zinaweza kuongeza mwonekano wa kipekee kwenye mavazi yake bila kuwa na mwonekano mzito.

Kwa ujumla, Rais Samia amekuwa kielelezo cha mavazi ya heshima yenye uzalendo na ushawishi. Wanampongeza kwa kudumisha asili ya Kiafrika katika uongozi wake na kuona kuwa mabadiliko madogo kama haya yanaweza kuleta mwonekano wa kisasa zaidi ambao unavutia na kuimarisha taswira yake kama kiongozi wa kimataifa.

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Oktoba 30- Novemba 5, 2024 |

## Kihimbwa haimbwi ingawa anang'aa



Na Mwandishi Wetu

KIUNGO mshambuliaji wa timu ya Fountain Gate, Salumu Kihimbwa anaendelea kung'aa akiwa na uzi wa kikosi hicho ingawa hatajwi sana miongoni mwa wachezaji wanaofanya vema kwenye Ligi Kuu ya NBC.

Nyota huyu mwenye umri wa Miaka 26 hadi sasa amehusika katika mabao 7 akifunga mabao matatu na kutoa pasi za usaidizi wa goli nne ndani ya Ligi Kuu ya NBC.

Kihimbwa nyota wa zamani wa Mtibwa Sugar ya Morogoro amekuwa sehemu ya mafanikio ya Fountain Gate msimu huu kwa kuziendesha puta timu pinzani sambamba na kufunga na kutengeneza mabao.





## Kelvin John 'anasota benchi' Denmark

AALBORG, Denmark

MTANZANIA Kelvin John amejikuta anasota benchi katika mechi tano mfululizo za mwisho ilizocheza timu yake ya Aalborg BK ya hapa Denmark.

Hadi sasa chama la nyota huyo linaloshiriki ligi daraja la kwanza limecheza mechi 13 ikiwa nafasi ya tisa kati ya 12 zinazoshiriki ligi na pointi 14 likishinda mechi nne, sare mbili na kupoteza saba.

Mara ya mwisho mshambuliaji huyo kuanza kwenye kikosi hicho ilikuwa Septemba 19 timu yake ikishinda mabao 4-1 dhidi ya Fredericia, John akifunga mabao mawili.

Baada ya kucheza dakika 90 ikiwa za kwanza tangu ajiunge na Aalborg BK msimu huu Septemba 23, timu hiyo iliheza dhidi ya FC Copenhagen ikipoteza kwa 2-0 na John akiwa benchi.

Tangu hapo amekuwa akisugua benchi na mechi ya mwisho timu hiyo imecheza Oktoba 25 dhidi ya Silkeborg ikitoa sare ya 1-1 'Mbappe' huyo wa Bongo akicheza kwa dakika tano.

Hata hivyo John anakutana na changamoto hiyo ya namba mbele ya mshambuliaji Mathias Jor-gensen raia wa Denmark ambaye ndio ingia toka kwenye kikosi hicho. Mpinzani wa Mtanzania huyu ana mabao sita kwenye mechi 13.

# Singida BS: Yanga wasije na matokeo mfukoni leo

## ●'Wananchi' wadai wamejichanga kupeleka mechi Zenji

Na Mwandishi Wetu

TIMU ya Singida Black Stars imewataka Yanga kutokwenda na matokeo yao uwanjani katika pambano lao la leo litakalofanyika katika dimba la Amani Complex Zanzibar kuanzia saa 2: 30 usiku.

Onyo hilo limetolewa na Afisa Habari wa Singida BS, Hussein Masanza kufuatia kile alichodai kuchoshwa na majigambo ya Yanga kwamba, wanakwenda kuwafunga katika mechi hiyo ya leo.

"Yanga na mashabiki wao wasije na matokeo yao mfukoni, huu ni mpira wa miguu kama kuna mtu anaenda kuweka bondi nyumba, mke au biashara yake kwamba Singida Black Stars lazima tufungwe basi awe tayari kwa lolote," ametahadharisha Masanza.

Masanza amewataka wapinzani wao Yanga wasijiamini kupitiliza wakaona mechi hii ni mechi ya kawaida, na kuwapasha kuwa, hawaongozi ligi kwa bahati mbaya bali ni kwa ubora wa timu yao.

Afisa habari huyo wa Singida BS ametanabahisha kuwa, wanafahamu wanaenda kucheza mechi ngumu na wanawaheshimu Yanga lakini wana uwezo wa kupambana hadi tone la mwisho na kushinda mechi hiyo.

"Nimesikia maneno ya Ali Kamwe mara kwa mara anazungumza kama anakuja kucheza na timu ya mtaani tu, achunge sana kauli zake maana hii mechi inakutanisha timu ambazo hazijapoteza mchezo hata mmoja msimu huu, tumeshasema inawezekana na tunamaanisha," amechimbwa mkwara Masanza.

Akijibu mapigo ya Masanza, Afisa Habari wa Yanga, Allya Kamwe amejinasibu kuwa, wana mafunzo mawili ya kuwapa Singida Black Stars, la kwanza ni kuwaonyesha kwa vitendo kuwa wamejichanganya kuipeleka mechi hiyo kwenye 'ngome' yao ya Zanzibar.

Kamwe amedai kuwa, Yanga ndio Mfalme wa Visiwa vya Zanzibar, hivyo Singida hawawezi kutoka salama. Pia wanakwenda kuhakikisha Uwanja wa Amaan unakuwa na rangi mbili tu, kijani na njano.

Msemaji huyo wa Yanga amelitaja funzo la pili wanalolitoa kwa Singida BS ni kuwaonyesha kuwa, msimamo wa Ligi Kuu huwa unapendeza pale Yanga inapokuwa kileleni, hivyo watatumia mechi hiyo kukaa kwenye nafasi 'yao' hiyo ya kileleni.

"Timu yenye mawazo ya ubingwa haiwezi kufurahia kuwa nafasi ya pili, ya tatu au ya nne, Yanga ilianzishwa kuwa nafasi ya kwanza





kuwa mabingwa, mchezaji anaposajiliwa anapewa hilo kwenda kupambana kulitimiza, Yanga tunatakiwa tukae nafasi ya kwanza tuwe mabingwa," Ally Kamwe Afisa habari Yanga.

Viingilio vya mechi hii ya leo ni shilingi 5000 (Jukwaa la Saa/ Orbit), shilingi 10,000 (Jukwaa la Urusi) shilingi 15,000 (Wings) na shilingi 20,000 upande wa VIP.



## Majaliwa: Wabunifu tunataka vazi la taifa



Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ametoa wito kwa wabunifu wa mavazi kukaa na kubuni vazi ambalo linaweza kutumika kama vazi la taifa.

Majaliwa ametoa wito huo Oktoba 27 alipokuwa akizungumza na jamii za watu wa Mkoa wa Kagera waliohudhuria Tamasha la Buhaya Festival huku akieleza kuwa, Wizara ya Sanaa na Utamaduni itapokea mavazi hayo na siku moja wabunifu watashindanishwa ili kupata vazi la taifa.

"Toka mwaka 2022 mpaka leo wanahangaika kutafuta vazi la taifa, Watanzania wabunifu ingieni kazini buni vazi la taifa halafu ipo siku tutakuja kushindanisha wasanii wabunifu ambao wamebuni vazi la taifa," ameagiza Majaliwa.

Wito huo umekuja baada ya kuwapongeza jamii za Kagera kwa uwepo wa mavazi maalumu ambayo yanawatambulisha na kutamani mchakato wa vazi la taifa ukamilike haraka ili kuwepo na utambulisho wa kimavazi kwa Watanzania.

Buhaya Festival ni Tamasha la Utamaduni ambalo linawakutanisha wazawa wa jamii za Kagera ambapo kwa mwaka huu 2024 wamekutana Mlimani City Dar Es Salaam wakionyesha tamaduni, vyakula na kujuzana fursa za kiuwekezaji zinazopatikana katika Mkoa wa Kagera.